Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TISA

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 30 Oktoba, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

*(Wimbo wa Taifa)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa kabla ya kuanza Kikao cha Bunge)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge ninapenda kuamini kwamba toka tulipoachana mmekuwa na afya njema na mafanikio katika shughuli zenu na sasa tuanze kazi ya kipindi hiki kwa muda wa wiki mbili. Lakini katika Mkutano wa Nane wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali Muswada wa kwanza ulikuwa *Appropriation Bill, 2012 na The Finance Bill, 2012.*

Kwa taarifa hii ninapenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba Miswada hiyo imekwisha pata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria za nchi zinazoitwa the

*Appropriation Act 2012 No. 7 of 2012* na *The Finance Act 2012, No. 8 of 2012*, kwa hiyo hii sasa ni Sheria.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA URATIBU NA BUNGE:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakaye tuulizia swali letu la kwanza ni Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli.

Na. 1

### Upandishaji Hadhi Vijiji Kuwa Miji Midogo

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi rasmi vijiji katika Tarafa ya Ikwiriri na Kibiti kuwa Mamlaka za Miji Midogo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthumu Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo umeainishwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 (13) ya mwaka 1982. Kwa mujibu wa Sheria hii vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa katika kuanzisha Mamlaka ya Miji Mdogo ni kama ifuatavyo:-

Kuwe na idadi watu wasiopungua elfu kumi (10,000), kuwe na na huduma za jamii zifuatazo; Shule ya Sekondari, Kituo cha Afya na Mhakam ya Mwanzo, kuwe na soko pamoja na maduka ya rejareja yasiyopungua matano (5) na eneo liwe Makao Makuu ya ata au Tarafa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vigezo hivyo, zipo pia taratibu zinazozingatiwa wakati wa kuanzisha Mamlaka ya Miji Midogo ambapo pendekezo la kuanzisha Mamlaka hizo lazima lianzie kwa wananchi wenyewe au kujadiliwa katika vikao vya Kisheria ambavyo ni Kamati ya Maendeleo ya Wilaya, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Lengo kubwa ni ushirikishwaji wa wananchi ili kupata ridhaa yao.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa zilizopo kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ni kwamba mapendekezo haya yameshajadiliwa katika vikao vya Baraza la madiwani na Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*). Kinachosubiriwa ni mapendekezo hayo kujadiliwa na kupata ridhaa ya Kamati ya Ushauri ya Mkoa ili yawasilishwe OWM-TAMISEMI kwa hatua zaidi.

Hivyo, mapendekezo ya kupandisha hadhi vijiji vya Ikwiriri na Kibiti kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo yakipitishwa katika vikao halali vya Kisheria, kukidhi vigezo na mihtasari yake kuwasilishwa OWM - TAMISEMI yatafanyiwa kazi pamoja na maombi mengine yaliyowasilishwa kwa

kuzingatia Sheria zilizopo. Aidha, zoezi la uhakiki wa vigezo na taratibu litafanywa na OWM - TAMISEMI kabla ya kuanzisha Mamlaka husika.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, kwanza tunashukuru sana Serikali kwa kuwa imepandisha hadhi Mji wa Utete na sasa imekuwa ni Mamlaka ya Mji Mdogo ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Ikwiriri ulitangazwa katika gazeti la Serikali toka mwaka 1996, na ilivyofika mwaka 2006 ramani ya mji ilikuwa tayari kwa ajili ya mji kupandishwa hadhi kuwa mji mdogo lakini mpaka sasa hivi ni kimya. Je, tatizo ni nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuruthumu Mchuchuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali ilitangaza nia ya kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ikwiriri na Kibiti lakini baada ya pale Halmashauri ilitakiwa ifuate zile taratibu ambazo zinafuata. Mpaka sasa ni kwamba Mji Mdogo wa Kibiti tayari umeshaandaliwa mpango kabambe lakini Mji wa Ikwiriri bado. Kwa hiyo, tunawaomba Mamlaka zinazohusika kukamilisha ile michakato ambayo iko kwao ili tuweze kuanza rasmi.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vigezo vyote vinavyohitajika ili kupandisha hadhi Kijiji cha Madaba kuwa Mji Mdogo vimekamilika na vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya watu, huduma, vikao vya *DDC*, *RCC* na vikao vingine vyote vimekwisha kamilika na tunachosubiri na tangazo la Serikali ili kijiji kile sasa kiwe Mji Mdogo na mambo mengine yaweze kuendelea.

Je, Mheshimiwa Waziri ananiambia nini mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho na hasa watu wale wa kijiji cha Madaba kwamba Serikali itatangaza lini kijiji kile kuwa ni Mji Mdogo maana imeshachukua muda refu sana mpaka sasa?

**SPIKA:** Wanaojua Madaba naomba Mheshimiwa Waziri ujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ukiwa Waziri wa Nchi TAMISEMI inabidi vijiji vyote ujaribu kuviweka kichwani, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo;-

Ni kweli kuwa vigezo vyote wameshakamilisha sasa hivi kazi iko kwetu Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kwenda kuhakiki mipaka ya eneo hilo ambalo sasa litakuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Madaba na kwa kushirikiana nao kwa pamoja kuhakikisha kuwa wanaandaa mpango kabambe wa Mji Mdogo wa Madaba, na

tutakapokamilisha tutautangaza rasmi Mji Mdogo wa Madaba.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika kijiji cha Lusewa Tarafa ya Sasawala, Kata ya Lusewa nayo hivyo hivyo taratibu zote zimefuatwa kama vigezo vinavyotakiwa kijiji kimezungumzwa na Kata, Wilaya na Mkoa RCC, lakini bado hatujatangaziwa kuwa Mji Mdogo ninaomba Mheshimiwa Waziri atufahamishe *position* ya Kata ya Sasawala.

**SPIKA:** Yaani Mkianza Vijiji vyote, haya Waziri unasikia *Dictionary.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo na ninaomba nijibu kwa wote kuwa taratibu ni zilezile na vigezo ni vilevile, wanapokamilisha upande wa Halmashauri sasa inakuwa ni zamu ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuhakiki mipaka. Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi katika kupima yale maeneo na kwa sasa hivi kazi ni kubwa sana, kwanza tuna kazi ya kuhakikisha kuwa tunahakiki mipaka ya Halmashauri za Miji na Wilaya ambazo tumezitangaza na ambazo hazijaanza.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo tunahakiki Mamlaka za Miji Midogo. Kwa hiyo, tunaenda hatua kwa hatua na

awamu kwa awamu. Ninaomba tu wawe na subira kazi tutafanya na tutakamilisha kwa wakati.

**SPIKA:** Kwa hiyo tunaendelea kwa sababu majibu ndiyo hayohayo, tunaendelea na Wizara ya Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, atauliza swali hilo badala yake Mheshimiwa Machali**.**

Na. 2

**Mpango wa Mkurabita na Utoaji Hati**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. FELIX F. MKOSAMALI)** aliuliza:-

Mpango wa MKURABITA na utoaji Hati *(Titles)* ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Muhambwe Wilayani Kibondo:-

(a) Je, ni lini ardhi itapimwa ili wapewe hati za kimila?

(b) Je, ni utaratibu gani utatumika kuchagua maeneo ya kupima ardhi kupitia MKURABITA?

(c) Je, ni kwa nini Hati za Nyumba zimekuwa na usumbufu kupatikana kwa wakazi wa Kibondo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mpango wa MKURABITA na utoaji wa Hati *(Titles)* ni muhimu siyo tu kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Muhambwe Wilayani Kibondo, bali kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kufuatia umuhimu huo na ukubwa wa nchi yetu, MKURABITA inatumia utaratibu wa kuwajengea uwezo wa Halmashauri za Wilaya na Miji katika kufanya urasimishaji kuwa wa haraka, rahisi na wa gharama nafuu. Halmashauri husika huchagua vijiji viwili ambamo urasimishaji unafanyika kwa ukamilifu kwa kushirikiana na MKURABITA.

Baada ya zoezi hilo, MKURABITA hutoa utaalamu na vifaa vya kufanyia kazi na Halmashauri inandaa Mpango wa Kurasimisha Wilaya nzima na kutafuta fedha hatimaye kuendelea na urasimishaji wa vijiji vinavyosalia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosambali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, upimaji wa ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ni sehemu ya mpango kazi wa muda mrefu (miaka kumi) ambao utekelezaji wake umeanza mwaka 2008/2009. Kutokana na mpango kazi huo wa muda mrefu umetengenezwa mpango kazi wa muda wa kati (miaka mitano) ambao utekelezaji wake umekuwa ukienda siyo kwa kasi sana kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imo katika upimaji wa ardhi wa mwaka wa fedha 2013/2014 kutokana na utaratibu nilioueleza katika maelezo ya utangulizi kadiri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika katika kuchagua maeneo ya kupima ardhi unazingatia vigezo vikuu vifuatavyo:-

Halmashauri kuonyesha utayari wa kufanya shughuli za urasimishaji.

Kuwepo kwa shughuli za Kiuchumi zitakazochochea matumizi haraka ya kiuchumi ya ardhi inayorasimishwa.

Kuwepo kwa watumishi wa kitengo cha ardhi wasiopungua wanne, katika fani ya upimaji, uchoraji na upangaji wa miji pamoja na Afisa Ardhi.

Kuwepo kwa masjala ya ardhi ya Wilaya na ya vijiji husika. Aidha, vijiji husika ni lazima pia viwe na vyeti vya Vijiji.

Idadi ya watu pia huangaliwa ili kufanya ukubwa wa matokeo *(Impact)* ya urasimishaji kuonekana zaidi.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu ugumu wa upatikanaji wa Hati za nyumba ni kwamba umilikishaji ardhi ya mijini unaongozwa na Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 ambayo bado ni ngumu na yenye taratibu ndefu. Maboresho ya Sheria na Kitaasisi yaliyopendekezwa na MKURABITA katika awamu ya pili yamelenga kubadilisha Sheria na mifumo ya kitaasisi ili umilikaji wa ardhi uwe rahisi, haraka na wa gharama nafuu. Kwa sasa Serikali iko katika mchakato wa kukamilisha maboresho hayo ili kuondoa usumbufu huo.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri ameeleza wazi kuwa Sheria namba 4 ya Mwaka 1999, inaonekana siyo nzuri sana kuwawezesha wananchi kuweza kupata Hatimiliki hasa zile za nyumba. Ningependa kupata majibu kwa niaba ya wananchi wa Muhambwe ni lini Sheria hii itarekebishwa maana yaliyotolewa ni ya jumla kuwa Serikali iko katika mchakato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu unakamilika lini ningependa tupate majibu ili tujue kwamba wananchi wataweza kunufaika lini na zoezi hili.

(b) Swali la pili, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kuwa kuna tatizo la fedha na ndiyo maana katika Halmashauri nyingi utakuta kwamba kuna baadhi ya Halmashauri hakuna hata mwananchi mmoja ambaye ana Hatimiliki ya viwanja pamoja na mashamba.

Mfano ni katika Wilaya ya Kasulu jambo hili linaonyesha wazi kabisa kuwa vitu vingine vinafanywa kwa uzembe ningependa kupata kauli ya Serikali, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya watumishi wa Idara ya Ardhi Wilayani Kasulu ambao hadi sasa tangu tumepata uhuru wananchi wanalalamika kuwa hakuna hata mwananchi mmoja mwenye Hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linatia aibu, ningependa kupata kauli ya Serikali kwa niaba ya wananchi wa Kasulu Mjini ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu lini mchakato utakamilika ninadhani ni wakati utakapokamilika kwa sababu mchakato wa kubadili Sheria wote tunaujua huwa unaanzia Serikalini na unaishia Bungeni. Kwa hapa siwezi kuweka tarehe ya lini Bunge hili litapokea marekebisho yanayohitajika, kwasababu marekebisho yafanyike na Serikali ikubali na inahusisha zaidi ya Wizara moja. Kwa hiyo, tuvute subira tutaleta mabadiliko wakati utakapofika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la uzembe kule Kasulu mimi sidhani kama ni uzembe ninachosema hapa ni kwamba liko tatizo la upatikanaji wa rasilimali fedha na Bunge hili ndilo linalogawa fedha na kila mwaka tunaleta maombi ya fedha na Bunge linaidhinisha. MKURABITA kwa mwaka inapewa shilingi kama bilioni tatu na shilingi bilioni tatu siyo fedha nyingi kuwezesha nchi yote kuweza kupimwa ndiyo maana tumeweka mkakati wa muda mrefu na mwuliza swali tulimwekea hata mwaka ambao tutapima katika eneo linalohusika.

Sasa kama kuna uzembe katika watumishi wa Kasulu hili suala kama ni uzembe kweli basi ule uzembe ushughulikiwe na mamalaka inayohusika kwasababu hawa watumishi wako chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

**SPIKA:** Ninaomba Jibu la nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya

nyongeza kuhusu swali la Mheshimiwa Mkosamali, kama ifuatavyo.

**SPIKA:** Hapana siyo Mkosamali ni swali la Machali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Spika kumradhi ni Mheshimiwa Moses Machali.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha itawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria mbalimbali za ardhi ili kuweza kukidhi mahitaji ya mabadiliko yaliyotokea toka sheria hizo zitungwe mwaka 1999 na marekebisho ambayo yamefanyika hadi kufikia mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusu gharama za upimaji wa ardhi, tumekuwa tukiwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba kwanza Halmashauri zinazohusika zitenge katika Bajeti zao fedha kwa ajili ya kugharamia sehemu ya gharama za upimaji wa ardhi na Wizara yangu ilikwishatoa taarifa kwamba pale ambapo Halmashauri ipo tayari sisi nasi tupo tayari kusaidia kwa watalaam pamoja na vifaa, lakini Halmashauri inayohusika iwe imejiandaa kwa fedha.

Pia wananchi washirikishwe kwa sababu gharama za kupima ardhi ya mwananchi ni ya mwananchi mwenyewe isipokuwa tunashauri kwamba ardhi ipimwe kwa pamoja ili kupunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante naona utauliza swali moja tu Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika nashukuru, katika maelezo yake na majibu Waziri ameleza changamoto kubwa ni uhaba wa rasilimali kuhusu utekelezaji wa MKURABITA na upimaji wa ardhi, lakini kwenye mwaka wa fedha uliopita 2011/2012 Bunge lilipitisha jumla ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya MKURABITA kwenye urasimishaji, na kati ya maeneo ambayo yaliyoainishwa kuwa yangekamilishwa upimaji eneo la Kimara Baruti katika Jimbo la Ubungo.

Kwa kuwa eneo hili fedha zilikuwepo tayari, lakini toka mwaka 2011 mpaka leo 2012 wananchi hawajapata Hati pamoja na kuwa fedha zilikuwepo.

Je, Waziri anachukua hatua gani kutokana na huo uzembe kwamba fedha zipo lakini Hati hazipatikani kwa wakati ili wananchi waweze kupata Hati na malengo ya msingi ya wananchi ya kupata Hati yafikiwe?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa alizozisema ni sahihi zinahusiana na ulipaji wa mishahara pamoja na gharama ya upimaji, bado hazitoshi. Lakini kama anazungumza *specifically* juu ya suala la upimaji katika eneo lile fedha hizi zimetengwa katika mwaka wa fedha ambao unaendelea.

Kwa hiyo Hati zitapatikana baada ya kuwa kila kitu kimeshakamilishwa. Nitafuatilia suala hili kuhakikisha kwamba zile Hati zinafika katika eneo analolizungumzia.

Mheshimiwa Spika, lakini labda niseme suala la jumla tu kwa Wabunge wote ambao wangependa kuona huduma hii ya MKURABITA inafanyakazi vizuri, niseme kwamba Halmashauri zijaribu katika Bajeti zake kutenga fedha ili huduma ya awali inayotolewa na MKURABITA ikimalizika Halmashauri ziendelee na kazi hiyo ili tuweze kufanikiwa.

Vile vile napenda kutoa wito kwa wale ambao wangependa kujifunza mafanikio ya kazi hii waende katika Wilaya ya Njombe ambako mimi nimeitembelea mwenyewe na kuona mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika urasimishaji wa eneo hilo. Unaweza kwenda ukajionea jinsi Wakulima walivyorasimisha mashamba ya chai na jinsi wanavyonufaika kutokana na *process* ya urasimishaji.

**SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuata la Wizara ya Fedha.

Na. 3

**Mapungufu ya Zoezi la Sensa**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kumejitokeza kasoro kadhaa katika maandalizi ya zoezi la Sensa ya mwaka 2012 kuanzia kwenye uteuzi wa Makarani wa Sensa na kukamilika kwa zoezi lenyewe:-

(a) Je, ni nini hasa chanzo cha kasoro hizo?

(b) Je, kwa nini maandalizi ya Sensa hayakufanyika vizuri wakati kulikuwa na muda wa kutosha?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya uhalisia wa takwimu zilizotokana na zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mapungufu ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi la mwaka 2012 yalisababishwa na utaratibu mpya wa kuwapata Makarani wa Kuhesabu Watu na Wasimamizi kwa njia ya ushindani badala ya kuwatumia walimu wa shule za Msingi, Sekondari na Watumishi wa Umma kama ilivyokuwa nyuma. Sababu zingine ni mitizamo tofauti ya kiitikadi kama sote tulivyokuwa tukifuatilia na vilevile badhi ya waombaji kukosa sifa.

Mheshimiwa Spika, mapungufu yaliyojitokeza yaliyotokana na malalamiko kutoka kwa baadhi ya waombaji wenye sifa ikiwa ni pamoja na wale wasiokuwa na sifa ambao walikosa nafasi. Kwa ujumla wao, walitoa malalamiko kwenye Vyombo vya Habari na sehemu zingine kwamba kulikuwa na upendeleo wakati wa uteuzi wa Makarani na Wasimamizi jambo ambalo lilikuwa sio kweli.

Uteuzi wa Makarani na Wasimamizi wa Zoezi la Sensa katika ngazi zote ulisimamiwa na Kamati za Sensa za Wilaya

zote nchini ambazo Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe. Kamati za Sensa za Wilaya zilifanyia kazi baadhi ya ya malalamiko halali na kazi ya kuhesabu watu ilifanyika kama ilivyopangwa.

(b) Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi yalifanyika vizuri licha ya changamoto chache zilizojitokeza wakati wa utekelezaji. Changamoto chache zilizojitokeza zilifanyiwa kazi na Serikali na zoezi la kuhesabu watu lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, ni wajibu wa kila mtu sasa kutimiza wajibu wake kama raia kwa lengo la kuliwezesha Taifa kutekeleza mipango yake kama ilivyopangwa.

(c) Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa shughuli ya kuhesabu watu, kazi inayoendelea ni kuingiza takwimu kwenye kompyuta, na kazi hii inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2012.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mbinu na tahadhari zote za kudhibiti uhalisia na ubora wa takwimu zilizochukuliwa wakati wa kipindi chote cha maandalizi na wakati wa kuhesabu watu ili kuhakilisha kwamba takwimu zilikusanywa zinakidhi viwango na ubora unaotakiwa kitaifa na kimataifa kama ilivyoainishwa kwenye *“United Nations, Guidelines for 2010 Round of Population Census”*.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba yapo mapungufu yaliyojitokeza kwa sababu ya utaratibu wa zoezi jipya la ushindani na kusababisha matatizo haya kutokea.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha kutokuwatumia walimu wenye uzoefu na kusababisha mapungufu haya kujitokeza?

(b) Yapo malalamiko ya Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ambao hawajalipwa posho zao mpaka leo, ni lini sasa Serikali itawalipa Viongozi hawa ambao walishiriki kwenye zoezi hilo la Sensa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kwanza tulifanya utaratibu mpya kwa kuwa Sensa ni zoezi ambalo tunataka kupanga mipango yetu ya baadaye, kwa hivyo tumefanya utaratibu mpya wa ushindani ili kuweza kuwapata hao ambao watakusanya *Data* pamoja na wasimamizi *through their qualification and through competition*. Kwa sababu tulikuwa tunataka tupate watu ambao wako mahiri kwa ajili ya zoezi hili.

Kwa hivyo haikuwa tu kama kawaida tunaweza tukachukua watu tu wakakusanya na takwimu baadaye zikawa hazipo kwenye *credit*. Kwa hivyo tumefanya hivyo kwa makusudi mazima ili kuweza kupata watu ambao wangeweza kabisa kulisimamia zoezi hili.

Hii ni mbali ya kuwakusanya wale watu lakini baadaye vile vile wakati wa *training* tumekuwa tukiwapa mitihani. Kwa hiyo wale ambao walipata chini ya alama hamsini tumekuwa tukiwaweka pembeni tunachukua ile *crème* ili kuweza kupata *Credible* Data kwa mipango yetu ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili kuhusiana na madai ya hawa Wenyeviti wa Mitaa, hili tunaendelea kulifuatilia na napenda tu kukuahidi kwamba hayo madai yote tayari sisi kama Wizara ya Fedha tumeyapata na tunaendelea kuyahakiki kwa ajili ya kuyafanyia malipo, Ahsante sana.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa inaaminika kulikuwa na kundi moja kubwa la dini moja kubwa hapa nchini halikushiriki katika zoezi zima la Sensa, kwa kuwa waumini hao kwa kupitia Viongozi wao waliarifu taasisi mbalimbali za kimataifa kwamba hawatashiriki na kwa kweli hawakushiriki.

Je, ni kwa vipi takwimu zetu za Sensa zitakubalika katika mizani ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kweli mwanzoni ilikuwa imetokezea kwamba kulikuwa kuna huo msimamo kwamba dini moja haitashiriki. Lakini napenda kukuhakikishia kwamba waumini wa dini hii wameshiriki katika Sensa hii na ni watu wachache tu ambao wameweka *propaganda* hii

ya kuwa zoezi la Sensa halijafanikiwa, lakini sisi kama Serikali tumeendeleana kampeni zetu na waumini wa dini hii mimi nikiwa mmojawapo nimeshiriki katika Sensa, Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana, katika swali ambalo limeulizwa juu ya Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji kutokulipwa hela kama ambavyo ilitegemewa kipindi cha zoezi la Sensa, nilitaka kujua ni kwanini imetokea hivyo wakati Serikali ilishatangaza kwamba watalipwa kiasi fulani na badala yake fedha hizo hazikupelekwa na hivi kupelekea hawa viongozi wetu kulalamikia sana Serikali yetu.

Je, nataka Serikali inipe jibu, ni kwanini kama Serikali ilishafanya Bajeti lakini baadaye ikaonekana tena fedha zile hazipelekwi kwa walengwa, ni nini kilichosababisha?

**SPIKA:** Haya na lini watalipwa, Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, swali hilo ni zuri na Mheshimiwa Kilufi anataka kujua ni kwanini wakati Bajeti ilikuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi Wabunge wote, kwanza kabisa tatizo lililojitokeza ni kwamba tuligundua dakika za mwisho kwamba wale watendaji wa Vijiji walikuwa hawatoshi kwa ajili ya kuunganisha maeneo yote ili tuweze kufanya kazi ile vizuri.

Kwa hivyo tukaongeza Wenyeviti wa Vijiji pamoja na wale Watendaji katika ngazi ya chini. Kwa hivi wale ambao walikuwa wanafanya kazi tuliwaongeza na hilo ndilo

lililosababisha tuchelewe kidogo kwa ajili ya kukamilisha malipo. Lakini kama alivyojibu vizuri Naibu Waziri, kazi hiyo tunamalizia na punde watu wote watakuwa wameshalipwa.

**SPIKA:** Ahsante tumechukua muda mwingi katika swali hili sasa tuende Wizara ya Maji. Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, atauliza swali hilo, hayupo Mheshimiwa Mtutura kwa niaba yake.

Na. 4

**Kuboresha Miundombinu ya Maji - Tunduru.**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MHE. ENG. RAMO M. MAKANI)** aliuliza:-

Miundombinu ya maji katika Mji wa Tunduru ni chakavu sana kiasi cha kusababisha ukosefu wa maji ya bomba safi na salama:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha na kuiwezesha Mamlaka ya Maji Tunduru itimize majukumu yake ambayo kwa sasa yamekwama?

(b) Je, ni lini Mji wa Tunduru utapata maji safi na salama ya kutosha kulingana na umri wa Mji huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala

Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Mamlaka za Maji katika Mji wa Wilaya na Miji midogo ukiwamo Mji wa Tunduru uliopo Daraja C unafanyika chini ya usimamizi wa Halmashauri husika. Halmashauri inapaswa kutenga fedha katika Bajeti zake za mwaka kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi, kugharamia shughuli za uendeshaji wa Mamlaka, kulipia gharama za umeme, na kugharamia ununuzi wa madawa ya kutibu maji.

Wizara yangu huzisaidia Mamlaka hizo katika uwekezaji wa miundombinu ya maji, kutoa ushauri wa kitalaamu na kuwajengea uwezo watumishi wake kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, Bodi za Mamlaka za Maji nchini ndizo zenye jukumu la kusimamia shughuli za uendeshaji wa mamlaka ili mamlaka hizo ziweze kutimiza wajibu wake. Uundwaji wa Bodi zinazosimamia Mamlaka za Maji katika Halmashauri hufanywa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Bodi ya Mamlaka ya Maji Tunduru imemaliza muda wake na mapendekezo ya majina ya Wajumbe wa Bodi ya Mamlaka hiyo yamewasilishwa TAMISEMI mwezi Septemba, 2012 kwa ajili ya uteuzi. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI mwezi Septemba, 2012 kwa ajili ya uteuzi.

Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI mwezi Septemba, 2012 kwa ajili ya uteuzi. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI itahakikisha kuwa Bodi ya Mamlaka ya Maji Tunduru inaundwa mapema ili iweze

kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utoaji wa huduma ya maji katika Mji wa Tunduru.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Mji wa Tunduru unapata huduma ya majisafi na salama, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*) imefanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji katika Mji wa Tunduru pamoja na miji ya Songea, Mbinga na Namtumbo.

Kazi ya usanifu wa miradi hiyo imekamilika na Makadirio ya gharama za ujenzi wa mradi wa maji Tunduru ni dola za Kimarekani milioni 12.62. Wizara yangu itaendelea kutenga fedha katika Bajeti zake za mwaka kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kadiri fedha zitakavyopatikana.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana, matarajio ya wananchi wa Tunduru na hata Mwuliza swali ilikuwa asikie kutoka Wizarani kwamba kiasi hicho cha fedha ambacho Serikali imekuwa ikitenga Tunduru imekuwa ikitengewa kiasi gani kwa sababu ndiyo msingi wa swali lenyewe.

Lakini hapa Wizara haijasema chochote, inasema kwamba Wizara itakuwa inaendelea kutenga fedha, fedha hizo Tunduru wananufaika kiasi gani?

Kwa hiyo, tunaomba Waziri ajipange upya atujibu swali hili vizuri atuambie Tunduru wamekuwa wakitenga hela, kwa sababu hii Wilaya ni kongwe sana, inasikitisha Boma toka mwaka 1907 leo mazingira yake ni magumu kuliko hata Boma ambazo zimeanzishwa hivi karibuni. Tunaomba Waziri ajipange upya atuambie ni kiasi gani cha fedha za

maji zinaelekezwa Tunduru katika ujenzi wa miundombinu kwa sababu hakuna chochote kinachofanyika kule hadi sasa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Haya, Naibu Waziri ujibu lakini amesema ujipange upya. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kwamba tatizo la maji lipo katika maeneo mengi ya Tanzania ikiwemo Wilaya ya Tunduru na Mamlaka ya Maji Tunduru. Tunazo Mamlaka 109 ambazo zote zinahitaji mafungu ya fedha kutoka Wizara ya Maji. Hivyo katika jibu langu la msingi nimesema kwamba tayari usanifu umeshafanywa na gharama za mradi kwa mamlaka ya maji Tunduru ni dola milioni 12.62.

Kwa hiyo, kazi ya kwanza imeshafanyika ya usanifu, kazi inayofuata ya pili sasa ni kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo ya maji. Kwa hiyo, siyo kwamba Serikali haijatenga fedha ni kwamba tayari imeshafanya kazi ya kwanza ya usanifu na fedha zimetumika kwa ajili ya ile kazi ya usanifu, hatua inayofuata sasa ni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu baada ya ile kazi ya kwanza kukamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza, aah! siyo ni Zainab Kawawa. (*Kicheko*)

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Taarifa za kiutendaji za Mamlaka mbalimbali za maji zinaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa sana la maji yanayovuja njiani zaidi ya kile kiwango cha kimataifa. Kiwango cha kimataifa kinataka uvujaji wa maji usizidi takribani asilimia 25, lakini kwa tathmini niliyoifanya binafsi inaonesha kwamba kwa wastani ukichukulia zile mamlaka zote inafika asilimia 45 mpaka 47 ya uvujaji wa maji, kwa hiyo kasi ile inaongezeka.

Wizara inachukua hatua gani ili kunusuru tatizo hili? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli maji yanavuja sana katika maeneo mengi, na kwa kiwango cha kimataifa kinatakiwa kisizidi asilimia 20.

Lakini mpaka sasa mamlaka nyingi ni kuanzia 30 na kuendelea kwenda huko juu ikiwamo hii Mamlaka ya maji Tunduru inazidi kwenye asilimia 45. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba mamlaka hizi zinasimamiwa uendeshaji wake na bodi, kazi ya Wizara yetu ni kutoa fedha kwa ajili ya uwekezaji, kwa ajili ya kutoa ushauri na mambo mengine.

Sasa suala hili la kudhibiti uvujaji wa maji lipo chini ya mamlaka, wanatakiwa wajipange wawe na mikakati ya kuhakikisha kwamba maji hayavuji. *(Makofi)*

Maji yanaweza yakawa yanavuja kwa sababu mbalimbali, mojawapo ni miundombinu mibovu ambayo inahitaji uwekezaji, kama nilivyosema kwamba kuna fedha zinatafutwa kwa ajili ya kuiboresha.

Sababu ya pili, inawezekana maji hayafiki kwa watumiaji kwa sababu watu ambao wanatumia hawajulikani. Hii ni kazi ya Mamlaka kuhakikisha kwamba kila anayetumia maji analipa. Namna pekee ya kuhakikisha maji hayapotei ni kuwafungia wateja wote dira au mita za kupimia yale maji. Kwa hiyo, ningetoa wito kwa Mamlaka za Maji nchini kutenga fedha kwa ajili ya kufunga mita ambazo wananchi wanaweza wakalipa maji sahihi kulingana na matumizi wanayotumia kwa kila mtu badala ya njia nyingine.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mahenge, kwa kusikia kilio chetu Wanangudu, tulipowataarifu kuhusu dharura ya maji walichukua hatua za haraka.

Naomba niulize swali kuhusu Sera Madhubuti ya Serikali inapotokea dharura ya maji hasa unapokuta wananchi wanatumia tope badala ya maji kama ilivyokuwa kwa Wananchi wa Kwimba.

**SPIKA:** Itakuwa maji ya tope, lakini tope kabisa haiwezekani! Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leticia Nyerere kama ifuatavyo:-

Kwanza, nashukuru tumezipokea hizo pongezi, lakini nijibu swali lake kwamba, baada ya kuona tatizo la maji katika Mji wa Ngudu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifanya ziara pale na aliacha maagizo kwamba Mamlaka ya Maji

na Halmashauri, watengeneze andiko waainishe matatizo yaliyopo ili fedha ziweze kutafutwa kwa ajili ya kutatua tatizo lililopo. Nilipopitia nimekuta andiko hilo wameshalitengeneza, limekwenda Mkoani linafanyiwa kazi ili kuondoa tatizo la maji pale Ngudu. (*Makofi*)

Na. 5

**Tatizo la Maji Katika Mji wa Ilula**

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA** aliuliza:-

Tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Ilula Wilayani Kilolo limedumu kwa zaidi ya miaka 25 bila kupatiwa ufumbuzi:-

Je, ni lini sasa Serikali itatoa ufumbuzi wa kudumu wa kero hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Peter Mahamoud Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika Mji Mdogo wa Ilula. Mahitaji halisi ya maji katika Mji huo ni mita za ujazo 2800 kwa siku, lakini uzalishaji wa maji kwa sasa ni mita za ujazo 821 tu. Katika jitihada za kuondoa kero ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Ilula, Serikali imeandaa mikakati ya muda mfupi na ya muda mrefu. Katika kutekeleza mikakati ya muda mfupi, Serikali katika kipindi cha mwaka 2007/2008 na 2008/2009, ilitumia jumla ya shilingi 230,299,000 kwa ajili

ya kazi zenye kuleta matokeo ya haraka (*Quick Wins*). Kazi zilizofanyika ni ununuzi wa mabomba na viungio vyake, ununuzi wa dira 260 za maji na ujenzi wa tanki lenye mita za ujazo 105.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mikakati ya muda mrefu, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*), imefanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika Miji ya Kilolo, Ilula, Makete, Mafinga, Ludewa, Makambako na Wanging'ombe. Makisio ya gharama yanaonesha kuwa ujenzi wa Mradi wa Maji katika Mji wa Ilula utagharimu shilingi bilioni 6.3. Serikali inaamini kuwa kukamilika kwa utekelezaji wa Mradi huo utakuwa ufumbuzi wa kudumu wa kuondoa kero ya upatikanaji wa majisafi katika Mji wa Ilula. Wizara yangu itaendelea kutenga fedha katika bajeti zake za mwaka ili Mradi huo uweze kutekelezwa.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika**,** nashukuru kwa majibu yenye matumaini, lakini napenda kueleza kwamba tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Ilula ni kubwa sana. Wakati Mji Mdogo wa Ilula unaanzishwa mwaka 1968, kulikuwa na wakazi 3000 tu, leo kuna wakazi zaidi ya 50,000 na mahitaji kama alivyosema Naibu Waziri wa Maji, kwa siku ni mita za ujazo 2800 na kwa sasa hivi maji yanayopatikana ni mita za ujazo 430 wala siyo 841:-

(i) Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kuweza kutatua tatizo hili?

(ii) Je, Serikali itakuwa tayari kutuma Wataalamu kuja kuangalia chanzo kingine cha maji ya mtiririko kilichoko katika Milima ya Serebu, Kata ya Image, kilomita 16, ili maji

yatoke huko na kuja Ilula kuondoa hii adha ambayo imedumu kwa zaidi ya miaka 23?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Peter Mahamoud Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kweli tatizo la maji pale Ilula ni kubwa kwa sababu wanatumia vyanzo viwili; kuna chanzo cha Ilomba ambacho kinatakiwa kizalishe mita za ujazo 259 na chanzo cha Idemule, chenye uwezo wa kutoa mita za ujazo 561 kwa siku, lakini kutokana na uharibifu wa vyanzo vya maji na kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, chanzo cha Ilomba hakitoi maji. Kwa sababu hiyo ndiyo maana imepunguza kutoka ujazo wa mita 821 kwenda kwenye hizo *meter cubes* anazosema 400, baada ya chanzo cha Ilomba kutofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la muhimu hapa la kutoa wito kwa wananchi wote, kutunza vyanzo vya maji, kwa sababu miundombinu ya huu Mradi ipo, lakini haina kazi kwa kuwa maji yamekauka kwenye chanzo. Kwa hiyo, hili nadhani ni funzo na wengine waanze kulinda vyanzo vya maji ili tusiwe na miundombinu ambayo haifanyi kazi. Kuhusu Mpango Mkakati, nadhani ndiyo huu ambao nimeuelezea kwamba, tayari Serikali ilishafanya usanifu katika Miji yote ya Mkoa wa Iringa, ambayo mingine sasa hivi ipo katika Mkoa Mpya wa Njombe na tukaainisha gharama zake kwamba ni bilioni 6.3 kwa ajili ya Ilula. Kwa hiyo, nadhani mkakati huo upo, unafanyiwa kazi, la msingi ni kutafuta fedha.

Ninakubaliana na swali lake la pili kwamba, tutatuma Wataalamu ili kuuweka Mpango huu ufanye kazi vizuri zaidi, tutapima vyanzo vingine vya maji ambavyo vitatumika kwenye kutekeleza huo mpango ambao tumeuanza. Bado tunawaomba wananchi waendelee kutunza vyanzo vya maji ili vitusaidie kwa muda mrefu zaidi.

Na. 6

## Serikali Kudaiwa na MSD Pamoja na Wazabuni

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA** aliuliza:-

Serikali inadaiwa na Stoo ya Madawa Nchini *(MSD)* kiasi cha shilingi bilioni 41 na pia Wazabuni mbalimbali wanaolisha Hospitali za Umma na Vyuo vya Uuguzi nao wanaidai Serikali:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inaathiri utendaji kazi wa MSD?

(b) Je, Serikali haioni kwamba hali hiyo inachangia wananchi wapate huduma za afya zilizo chini ya viwango?

(c) Je, Serikali haioni kwamba hali hiyo huchangia Vyuo vya Afya kutoa huduma mbovu za chakula kwa wanafunzi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Rosweeter Faustin Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa deni la kiasi cha shilingi bilioni 41 ilizokuwa ikidaiwa na Bohari ya Dawa Nchini (*MSD*). Ni kweli kuwa deni hili linaathiri utendaji wa *MSD*. Kwa kiasi kikubwa, hali hii imesababishwa na ufinyu wa bajeti kila mwaka. Serikali imeendelea kupunguza deni hili kadiri hali ya fedha inavyoruhusu. Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Oktoba, 2012, deni hili limepunguzwa na kufikia kiwango cha shilingi bilioni 36. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imewasilisha Wizara ya Fedha ombi la kulipwa kwa deni hilo na ombi hilo limekubaliwa. Hivyo, Serikali italipa deni hilo pale fedha zitakapopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua jukumu lake katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata huduma bora za afya. Ili kutimiza jukumu hili ipasavyo, Serikali imekuwa ikiongeza mgao wa fedha kwa ajili ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kadiri ambavyo mapato yake yamekuwa yakiongezeka. Aidha, Vituo vya Umma vya Huduma za Afya vinaruhusiwa kununua dawa nje ya mfumo wa *MSD*. Kwa mwaka huu wa fedha 2012/13, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 268,530,025,036 kwa ajili ya kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Umma, ikilinganishwa na shilingi bilioni 181,477,959,040 ilizotumia mwaka 2011/12, kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Vituo vya kutolea Huduma za Afya vya Umma. Wizara imeendelea kuhamasisha Hospitali kwa kupitia Mfuko wa Bima ya Afya, kutumia fursa iliyotolewa ya kuweza kupata mkopo kutoka Bima ya Afya wa kununulia

mahitaji ya kuboresha majengo pale fedha zinazotolewa na Serikali zinapokuwa hazitoshelezi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua madeni yanayotokana na huduma walizotoa wazabuni mbalimbali katika Vyuo na Hospitali. Madeni haya yanatokana na ufinyu wa bajeti na ulazima wa huduma hizo kuendelea kutolewa katika Hospitali na Vyuo. Madeni hayo yanatokana na bajeti isiyotosheleza kununulia chakula cha wanafunzi Vyuoni na wagonjwa Hospitalini. Hata hivyo, Serikali inaendelea na jitihada za kupunguza madeni hayo ili kuboresha huduma katika Vyuo na Hospitali kwa kuongeza bajeti na kadiri fedha zinapopatikana. Ili kuhakikisha kwamba huduma ya chakula inaendelea kutolewa kwa wanafunzi, Serikali imeongeza bajeti ya chakula kuanzia mwaka 2011/12 ya shilingi 2,500,000,000 na mwaka 2012/13 kufikia shilingi 3,500,000,000.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mpaka sasa hivi nikizungumza deni la MSD ni shilingi bilioni 39.8 na inavyoonekana ulipaji wa deni hili kasi yake ni ndogo mno:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba inaathiri *MSD* katika uwezo wake wa utendaji kazi wa kununua madawa, kusambaza na kufuatilia mpaka kwenye vituo?

(b) Azimio la Abuja limeagiza Wizara ya Afya itengewe asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali katika kuondoa matatizo kama haya. Je, Serikali itatilia lini maanani na kutekeleza hili Azimio la Abuja ili kuwapa Wizara ya Afya bajeti ya asilimia 15 ili matatizo haya yaweze kuondoka na

wananchi waweze kupata huduma bora za afya na hasa kundi la wanawake, watoto na kundi la wazee? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasikila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, deni la *MSD* tunalitambua wote, limetokana na madawa ambayo yamekuwa yakiingizwa nchini katika mfumo wa msaada na kutotengewa fedha kwa ajili ya kugomboa na gharama zake nyinginezo na ndiyo sababu deni hili limekuwepo. Kwa vile tumeshawasilisha Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha imekubali kuliingiza hili deni katika kulilipa, mimi naamini tuipe muda Serikali iweze kulilipa hilo deni.

Suala la *MSD* kutofanya kazi vizuri kwa sababu ya hili deni, itakuwa mchango wake ni mdogo sana kwa sababu fedha ambazo wanapokea ni nyingi za kuweza kuwatosheleza kufanya hizo kazi. Kwa hiyo, naamini katika kipindi ambacho Serikali itaweza kukamilisha hilo deni, basi *MSD* itaendelea kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Azimio la Abuja la asilimia 15, bajeti yetu ya Wizara ya Afya imekuwa ikipanda na kushuka kwenye wastani wa asilimia 10 mpaka 11, lakini kufikia asilimia 15, itategemea tu pale ambapo uwezo wa Serikali utakuwa umeweza kutufikisha pale. Vile vile inategemea na vipaumbele ambavyo sisi wote Bungeni hapa na Serikali tutaamua kuvitoa. Tunapoamua kutoa vipaumbele kwenye maeneo ya ujenzi maana yake ni kwamba ni lazima tupunguze *share* ya *percent* ambayo itaingia katika Wizara

nyinginezo. Kupanga ni kuchagua, hivi sasa tumo katika kuhakikisha bajeti inaendelea kukua, lakini kama Wizara, imekuwa ikiangalia mifumo mbalimbali ya kuweza kujitosheleza kwa kutafuta njia mbadala ya kujipatia fedha ikiwemo ya Bima ya Afya ambayo sasa hivi inatekelezeka hapa nchini.

Na. 7

**Ubora wa Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari**

**MHE. JAMES F. MBATIA** aliuliza:-

Kwa zaidi ya miaka kumi sasa Serikali imekuwa ikibadilisha Mitaala ya Shule za Msingi na Sekondari, hali ambayo haiwaridhishi wadau wengi wa elimu kwa kuwa ubora wa elimu unashuka na inakuwa siyo endelevu:-

Je, Serikali ina msimamo gani kuhusu suala zima la Mitaala ya Elimu ya Shule za Msingi na Sekondari kutokuwa na ubora unaostahili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya Mitaala na maboresho yake ni mchakato endelevu, ambayo hufanywa kwa kuzingatia taarifa za kiutafiti kuhusu mahitaji ya jamii, ukuaji wa sayansi na teknolojia, ufundishaji na

ujifunzaji kwa ngazi husika, matamko mbalimbali ya Kimataifa na Kitaifa na Mzunguko wa Maboresho ya Mitaala (*Review Cycles*) kwa kila ngazi husika.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya Mitaala ya Elimu nchini yamefanyika mara nne tu tangu tupate Uhuru. Mabadiliko hayo yalifanyika kwa mara ya kwanza mwaka 1967 ili kubadili mfumo wa elimu kutoka ule wa Kikoloni na kuweka wenye mtazamo wa Kitanzania kwa kuzingatia dhana ya Elimu ya kujitegemea. Mwaka 1979 mabadiliko yalihusisha uanzishwaji wa shule za michepuo ya ufundi, biashara na kilimo ili kutekeleza kwa vitendo Elimu ya Kujitegemea na Sera ya "Siasa ni Kilimo".

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 mabadiliko ya Mtaala yalipunguza uwingi wa masomo ya Elimu ya Msingi kwa kuanzisha masomo ya Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi. Katika mwaka 2005 mabadiliko yalihusu Ufundishaji na Ujifunzaji unaozingatia Ujuzi (*Competence Based Teaching and Learning*), pia uanzishwaji wa masomo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), Haiba na Michezo kwa Elimu ya Msingi. Mabadiliko yote hayo yanalenga kutoa wahitimu wenye ujuzi stahiki kwa kila ngazi na kwa mahitaji ya wakati uliopo ili kuweza kumudu mazingira yao na ushindani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ubora wa elimu hupimwa kwa vigezo mbalimbali kama vile Mtaala wenyewe na taratibu za upimaji na tathmini yake, taratibu za ufundishaji na ujifunzaji, usimamizi na uendeshaji na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge lako Tukufu kwamba Mtaala unaotumika sasa ni ule wa Mwaka 2005; na kwa kuwa kuna hisia kwenye jamii kwamba Mitaala hii imekuwa ni jambo la siri wakati elimu siyo jambo la siri wala siyo jambo la kuficha. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuleta Mitaala hii kila Mbunge apate *copy* yake katika Mkutano huu wa Bunge ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufuatilia Mitaala hii kwa urahisi katika Mashule ya Sekondari na Shule za Msingi? (*Makofi)*

(b) Kwa kuwa katika majibu yake amesema Mtaala wa Mwaka 2005 unamwezesha mwanafunzi katika viwango mbalimbali ili aweze kushindana Kimataifa; na kwa kuwa hivi sasa kuna wanafunzi ambao wanamaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika; na kwa kuwa chanzo kikubwa cha wanafunzi hao kutokujua kusoma na kuandika ni pale mtoto anapoanza darasa la kwanza badala ya kusoma masomo matatu tu ambacho ni kiwango cha Kimataifa, yaani KKK; Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, lakini mtoto wa darasa la saba leo hii hapa Tanzania anasoma masomo manane; kusoma, kuhesabu, kuandika, jiografia, hisabati, stadi za kazi, elimu ya uraia na haiba ya michezo:-

Wizara haioni kwamba inam-*frustrate* mtoto huyu siku ya kwanza ya kuanza masomo na ndiyo maana wanafunzi wanamaliza darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika?

Kwa nini Serikali *immediately* isirudishe masomo matatu, yaani KKK ili tuweze kwenda sambamba na viwango vya

Kimataifa na Taifa letu liweze kuwa na watu wenye kufikiri vizuri na wenye *power of reasoning* nzuri? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, labda nieleze dhana halisi ya neno *Curriculum* na *Syllabus,* yaani Mtaala na Mihtasari. Mtaala ni neno pana, ni dhana kubwa, lakini *Syllabus* ndiyo hizo ambazo zinatumika kwa Walimu, kwa ajili ya kutengenezea miongozo ya kufundishia madarasani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, anapenda kuliomba Bunge lako Tukufu liridhie Wizara ya Elimu isambaze Mitaala kwa kila Mbunge kwenye Bunge hili. Mimi sina matatizo na hilo, lakini basi niahidi kwenye Bunge lijalo kwamba, tutachapisha Mitaala hiyo ya Elimu ya Mwaka 2005, tutawagawia Wabunge, waweze kuona dhana kamili ya neno Mtaala *(Curriculum),* kuna nini ndani yake *(Content),* halafu baadaye tuje tuone namna Walimu wanavyochukua Mtaala kwenda kwenye Mihtasari; *Curriculum to Syllabus,* ndipo angalau tutaweza kuelewa jambo halisi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi dhana iliyopo huko kwenye Jamii ni kwamba, Wizara au Serikali, inabadilisha Mitaala mara kwa mara; kama nilivyosema, tumebadilisha Mitaala mara nne tu toka tupate Uhuru. Hata ukienda kwenye nchi nyingine wanatucheka sana Watanzania kwamba, mbona hatubadilishi, hatuendani na

wakati unavyokwenda. Kwa sababu, Dunia inapobadilika yapo mambo ya *cross cutting issues* katika jamii yanaingiliana; mambo ya UKIMWI, mambo ya Mazingira, kumbe ni lazima watoto wale uwafundishe kutokana na dunia inavyokimbia na wewe unakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu hizi KKK; mimi sina ubishi na Mheshimiwa Mbatia na si Mheshimiwa Mbatia tu, Wabunge wote wamekuwa wakilieleza hili. Hata sisi tumeshaanza Vikao vya Menejimenti pale Wizarani chini ya Mheshimiwa Waziri, tunalitazama kwa kina sana. Tayari tumeshapata Kamishna pale Wizara ya Elimu, tumekaa miaka mitatu hatuna Kamishna. Tumeshaanza Vikao vya kuangalia ni namna gani tumuweke mtoto wa darasa la kwanza na la pili aweze kusoma zile KKK; kusoma, kuandika na kuhesabu, baada ya hapo tutaweza kuona mtoto huyu wa darasa la kwanza anajua kusoma ili akifika darasa la saba, awe na *knowledge* ya kusoma, kama ulivyoshauri Mheshimiwa Mbatia.

Na. 8

**Ujenzi wa Chuo cha Ufundi – Rorya**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi *(VETA)* Wilayani Rorya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Wilaya nchini, Serikali itajenga vyuo vipya na kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(Folk Development Colleges – FDCs),* kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika ngazi za Wilaya. Aidha, katika kutekeleza mpango huo, kipaumbele kinatolewa kwa kuanza na wilaya ambazo hazina Vyuo vya Ufundi Stadi vya Serikali ama visivyo vya Serikali au Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rorya ni miongoni mwa Wilaya zilizokwishafanyiwa utambuzi wa stadi na ipo katika awamu ya pili ya mpango wa ujenzi wa vyuo vipya vya ufundi stadi. Namshauri Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Rorya, watumie Chuo cha Ufundi Stadi cha Mara, wakati Serikali ikiendelea na jitihada za kutafuta fedha za ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Ninataka awaeleze Wananchi wa Rorya ni lini Chuo cha *VETA* kitajengwa Wilayani humo?

(ii) Naomba vilevile awaeleze Wananchi wa Tarime ni lini Chuo cha *VETA* kitajengwa Wilayani Tarime na siyo kutegemea Chuo cha Musoma?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyangwine, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda hapa nieleze tu kwa Wabunge wote wanaokuwa na maswali haya ya *VETA* kwenye Wilaya zao; ni kweli kama tulivyozungumza kwenye bajeti kwamba, Serikali iliahidi kujenga vyuo vipya vya *VETA* katika kila Wilaya kwa zile Wilaya ambazo bado hakuna Vyuo vya *VETA.* Kwa ujumla, Wabunge wengi tu wangependa kusimama hapa kuulizia ni lini Wilaya zao zitapata fedha za kujengewa Vyuo vya *VETA* na mwaka huu tumetenga Wilaya nne.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ni kwamba, Serikali inaendelea na mazungumzo na kuandika maandiko mbalimbali kwa wenzetu wa China na tumeshaanza mazungumzo mazuri tu angalau tuje tupate fedha kwa pamoja, tujenge *VETA,* ikiwezekana zote kwa wakati mmoja. Hii ya kupanga kwa kila mwaka *VETA* vyuo viwili, vitatu au vinne, hatutaweza kufika tunakotaka kufika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu Wabunge wawe wavumilivu, Serikali imeshaanza mazungumzo na Wahisani, tutaweza kukopa fedha kwa riba ndogo na kuweza kujenga Vyuo Vya *VETA.* Lini Rorya au Tarime? Ni mjumuisho wa hizi Wilaya zote siku hiyo tutakapokuwa tumepata fedha.

Na. 9

## Kubadilika kwa Mifumo ya Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo

**MHE. JITU V. SONI (K.n.y. MHE. ROSE K. SUKUM)** aliuliza:-

Serikali ilianzisha mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo kama mbolea na mbegu kwa kuingia mkataba na makampuni kabla ya kuanzisha mfumo mpya wa matumizi ya vocha za pembejeo za kilimo katika msimu wa mwaka 2008/2009; na mwaka 2012/2013 Serikali ilibadili tena mfumo huu wa vocha na kurudia mfumo wa zamani wa kutumia kampuni:-

(a) Je, kuna tatizo gani linalosababisha Serikali kubadili mifumo ya usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima?

(b) Je, kubadili mifumo ya usambazaji kunaweza kuondoa matatizo sugu ya rushwa na ufisadi yanayosababisha pembejeo kutowafikia wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikibadili mfumo wa utoaji ruzuku ya pembejeo kwa wakulima ili kuongeza

ufanisi na kukabiliana na changamoto mbalimbali za utekelezaji. Aidha, utaratibu wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima kwa njia ya zabuni kupitia makampuni ya pembejeo ulitumiwa na Serikali kati ya mwaka 2003/2004 hadi 2007/2008 na ulibadilishwa kutokana na changamoto nyingi, lakini zifuatazo naomba niziainishe:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, pembejeo kutowafikia wakulima walengwa (Wakulima Wadogo) badala yake walionufaika ni kampuni na mawakala wa pembejeo. Pili, kiwango cha udanganyifu kilikuwa kikubwa kwa sababu aina moja ya pembejeo ilikuwa na bei mbili, yaani yenye ruzuku na isiyokuwa na ruzuku, hivyo kuwa rahisi kwa mawakala kudanganya wakati wa kuifikisha kwa wakulima. Tatu, kwa maeneo ya pembezoni mwa nchi, pembejeo hazikuwafikia wakulima kwa wakati mwafaka na pia kulikuwa na utoroshaji wa mbolea nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kasoro hizo, Serikali iliamua kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wa mazao ya chakula (mahindi na mpunga), kwa kutumia mfumo wa vocha kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2012/2013. Aidha, pamoja na mafanikio chini ya utaratibu wa vocha kwa kuongezeka kwa tija kwenye mazao hayo, kwa kuboresha usalama wa chakula, bado baadhi ya changamoto zimeendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, msimu wa 2012/2013, makampuni ya pembejeo ndiyo yatakayoteua mawakala wa pembejeo na kukabidhi kwa Kamati ya Pembejeo ya Wilaya kwa ajili ya uhakiki. Utaratibu huu unatarajia kupunguza udanganyifu wa

mawakala kwani wakala atalazimika kuuza pembejeo ambayo ndiyo shughuli yake kuu ya kampuni anayoiwakilisha. Aidha, pembejeo zitawahi kuwafikia wakulima, sambamba na kuondoa matatizo sugu ya rushwa na pembejeo zisizokidhi kiwango kwani kampuni husika iliyomteua wakala itawajibika. Lengo ni kuwawajibisha mawakala kuhusu udhibiti wa ubora wa pembejeo wanazowauzia wakulima.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naipongeza Serikali, kwa mfumo huu mpya ambao wameubadilisha na kuhakikisha kwamba, sasa pembejeo itawafikia Wakulima na ule mwanya wa kuchakachua hautakuwepo. Ninaomba kuiuliza Serikali maswali yafuatayo:-

(i) Je, wamejiandaa vipi kutoa elimu kwa wananchi kuhusu huu mfumo mpya ili wasije kubabaika na pasiwe na mwanya wowote mwingine utakaojitokeza?

(ii) Je, ni lini Serikali itaangalia uwezekano wa kuweka ruzuku katika pembejeo hasa katika masuala ya umwagiliaji katika zana za umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Jitu Soni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimshukuru Mheshimiwa Jitu Soni, kwa kutambua kwamba, mfumo huu wa vocha wa hivi sasa unahitaji mabadiliko kwa lazima; kwa sababu changamoto zilizokuwepo zilikuwa

zinatupeleka kwenye *stagnant situation* ambayo isingeweza kukuza kilimo kwa hatua hii iliyofuatia.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu, maelezo ya mfumo wa ruzuku wa pembejeo kwa mkopo ambao ndiyo unatakiwa kuanza 2013/2014; tutakuja kwenye Bunge lako Tukufu na kuwafahamisha Wabunge kwa kina kuhusu mfumo huu mpya, kwa sababu inatakiwa sisi sote tuuelewe ili uweze kutekelezwa. Kimsingi, misingi yake ni kuweza kuwakopesha, mkulima anawajibika kukopa kupitia kikundi cha ushirika na kikundi kile kitakuwa kinatoa asilimia 20 na ule mkopo utakuwa na riba ya kiasi cha asilimia nane kutoka Taasisi za Fedha.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, wakulima wadogo watakaokuwa kwenye kile kikundi, watapata manufaa ya kupata pembejeo kwa wakati na zenye ubora zaidi. Kimsingi, mfumo mzima tutakuja hapa Bungeni na kuuelimisha zaidi, pamoja na kupanua wigo wa aina ya pembejeo zitakazohusika kwenye mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Jitu Soni, lazima tuwapatie wakulima wenyewe elimu ya msingi juu ya mfumo utakavyokuwa na kadhalika ili kuondoa changamoto zilizopo. Kwa hiyo, tumejiandaa, tumekadiria tutakuwa na changamoto kubwa kama nne au tano hivi, ambazo tayari tumeanza kuzifanyia kazi hivi sasa. Kwa hivi sasa bajeti ya elimu kwa wakulima tumeiongeza ili utaratibu huu wa vocha uweze kueleweka vizuri zaidi kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la vifaa vya umwagiliaji, ninaamini Mheshimiwa Jitu, alikuwa na maana ya ruzuku kwenye vifaa vya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kuongeza matumizi ya umwagiliaji kwa kilimo, unaongeza uzalishaji na tija kwa wakulima. Kwa hiyo, kama ilivyokusudiwa kwenye vifaa vya trekta na zana za kilimo, tunaweza tukaangalia namna ambavyo vifaa vya umwagiliaji vitaingia katika mfumo, katika *package* kubwa ya vifaa vya *mechanization,* zana za kilimo, ili ziweze kupata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tulifanyie kazi kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha. Nakushukuru.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, toka mwaka 2007, tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya Wizara ya Kilimo, kuhusiana na ruzuku ya mbolea za wastani wa shilingi bilioni 60 kila mwaka. Toka mwaka 2007 mpaka sasa zimekuwa zikiongezeka na kupungua, lakini wastani ni wa shilingi bilioni 60. Imegundulika dhahiri kabisa kwamba, fedha hizi zimekuwa zikiibwa na watu wanaohusika wa Serikali na Mawakala binafsi ambao wanahusika na mbolea.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Tano wa Bunge wa mwezi Novemba, 2011, Waziri wa sasa wa Kilimo, ambaye wakati huo alikuwa Naibu Waziri wa Kilimo, alipokuwa akijibu Swali la Mheshimiwa Raya, kuhusiana na uchakachuaji wa mbolea ya ruzuku katika Mikoa ya Mbeya na Rukwa, alisema kwamba; Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anafanya ukaguzi maalum kuhusiana na fedha zilizotengwa kwa mbolea ya ruzuku na namna gani

ambavyo zimetumika. Ninaomba Serikali itoe kauli hapa Bungeni, uchunguzi huo na ukaguzi huo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, umefikia wapi, Taarifa yake iko wapi na ni lini utafikishwa Bungeni ili tuweze kuona ni namna gani ambavyo tutashughulikia suala la wizi wa fedha za umma katika mbolea ya ruzuku?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tulimwomba *CAG* afanye ukaguzi kufuatia wimbi kubwa la wizi na hujuma za vocha, lakini kazi hiyo bado haijakamilika. Kwa hiyo, siwezi kusema sasa nitaleta majibu yale, lakini kazi itakapokamilishwa na *CAG,* basi tutawapa majibu ambayo *CAG* atakuwa ametupatia.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, kumekuwa na kesi zinapelekwa Mahakamani kila wakati. Hata sasa zipo kesi 44 ambazo zipo Mahakamani, zinazohusiana na wizi na hujuma wa pembejeo; hizo, nyingine zimeshahukumiwa, lakini hilo la *CAG* kazi ikikamilika nitaleta majibu.

Na. 10

**Pembejeo na Ruzuku kwa Wakulima**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Pembejeo na ruzuku za kilimo zikitumiwa vizuri zinaweza kuwakomboa wakulima kutoka kwenye lindi la umaskini:-

(a) Je, wakulima hasa wa vijijini wameelimishwa kiasi gani kuhusu pembejeo na ruzuku zitolewazo kwa wakulima?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isiwakopeshe wakulima pembejeo na ruzuku wakati wa msimu na marejesho yafanyike baada ya mavuno?

(c) Je, Serikali, inafahamu kuwa wakulima huhujumiwa pembejeo na ruzuku zao na watendaji na inachukua hatua gani dhidi yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Jimbo la Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya, kupitia Maafisa Ugani walioko katika Kata na Vijiji, inaendelea kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya pembejeo na utoaji wa ruzuku ya pembejeo. Aidha, njia mbalimbali kama vipeperushi, magazeti, mikutano ya hadhara, redio, sinema, televisheni na Maonesho ya Nane-Nane, Wiki ya Utumishi wa Umma na Wiki ya Ushirika, hutumika pia katika kutoa elimu kwa wakulima.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wakulima unafanyiwa maandalizi ili

uanze kutumika mwaka 2013/2014. Nazikumbusha Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya, kuwaandaa wakulima kwa kuwahamasisha kujiunga kwenye vikundi ili waweze kukopesheka kwenye taasisi za fedha kwa kuzingatia utaratibu uliotolewa kwenye Mikutano ya Kanda, mwezi Julai hadi Agosti, 2012.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwachukulia hatua za Kisheria na kinidhamu Watumishi wa Serikali na Mawakala wadanganyifu; mathalani mwaka 2009/2010, jumla ya kesi 22 zilifunguliwa Mahakamani. Mwaka 2010/2011 jumla ya kesi 44 zilifunguliwa na baada ya kubaini mapema dalili za udanganyifu wa malipo kwa mawakala, malipo yamesimamishwa katika Mkoa mzima wa Mara, Wilaya ya Loliondo na Wilaya ya Kilosa. Aidha, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na TAKUKURU, uchunguzi wa udanganyifu unaendelea katika Wilaya za Lushoto na Kigoma Vijijini.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ambazo huchukuliwa ni pamoja na kuzuwia malipo ya Mawakala wa Pembejeo, wanaothibitika kufanya hujuma ya utoaji wa ruzuku ili kupisha uchunguzi na pale inapobainika, wahusika hufikishwa Mahakamani. Aidha, Serikali inasisitiza usimamizi madhubuti katika ngazi za Kamati za Vocha za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Mkoa wa Mara umetajwa kwamba, umeshamiri sana kwa udanganyifu wa Mawakala ambao wanasambaza pembejeo; na kwa kuwa hali hii imesababisha wakulima wa Mkoa wa Mara kunyanyasika na hadi sasa inaonekana hawa watu adhabu waliyopewa ni kunyimwa au kusimamishiwa malipo. Je, hiyo adhabu inatosha; kwa nini hawa watu wasihukumiwe kama Wahujumu Uchumi na wafungwe jela?

(ii) Mkoa wa Mara una bahati ya kupata misimu miwili ya mvua kwa mwaka; kuna msimu ambao ni wa masika na kuna msimu ambao ni wa mvua za vuli, lakini inaonekana kabisa kwamba, pembejeo zinaenda wakati wa msimu wa mvua ya masika. Serikali, ina mpango gani kuhakikisha wakati wa msimu wa mvua ya vuli inapeleka pembejeo ili kuwasaidia wakulima wanaopanda katika msimu huo?

Mheshimiwa Spika, kwanza labda niseme tu kwamba, pale kwenye kusisitiza kuhusu udanganyifu na wizi uliokuwa unafanywa na Mawakala, labda sikujielekeza vizuri, lakini kwenye swali sikumaanisha kwamba, ulikuwa umeshamiri Mkoa wa Mara tu. Kusema kweli mfumo mzima wa usambaza wa vocha za pembejeo umeshamiri kote, Mawakala wengi walikuwa wanajishusisha katika mfumo huo wa udanganyifu na hasa kwa kuwashirikisha saa nyingine hao wakulima wenyewe. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba tulikuwa hatupati ufanisi uliokuwa unatakiwa, ndiyo maana tumesema, tunakwenda kwenye mfumo mpya ambao kwanza, Mawakala watakuwa wanawajibika wenyewe. Lakini pili, tutakuwa tunatumia mfumo wa kusambaza kwa mkopo pembejeo hizo ili pawe na kuwajibika zaidi kwa mkulima pia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba, hii hukumu ya wahujumu uchumi kwa upande wa Mawakala wanaofanya udanganyifu wa pembejeo, nakubaliana naye, kusema kweli kwa sababu hili tunaliona hata kwenye matumizi ya mbolea na wauzaji wa mbolea feki na mbolea zinazochakachuliwa, nadhani nao wangeingia kwenye wahujumu uchumi na tunalifanyia kazi Serikalini ili kuwapa adhabu kali zaidi wale ambao wanatengeneza utajiri kwa kuwafanya wakulima maskini zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, kuhusu suala la msimu wa masika, ugawaji wa pembejeo unasubiri upandaji mkubwa na hata hivi sasa vocha ziko tayari kule Mkoa wa Mara na ziko kwenye ngazi ya Wilaya. Tunatambua kwamba kuna tatizo la usambazaji wa vocha mwaka huu, nyingi zimekwama kwenye hatua ya Mkoa na Wilaya, lakini fikra ni kuzipeleka wakati ambapo wakulima wanakuwa na matumizi makubwa zaidi ya pembejeo ambao ni wakati wa kusubiri mvua za masika.

**SPIKA:** Naomba tuendelee kwa sababu tuko nyuma sana ya muda. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia! Atakayeuliza swali ni Mheshimiwa John Paul Lwanji!

Na. 11

**Kampuni ya *AIRTEL* Kujenga Mnara wa Simu**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu iliyotolewa na kampuni ya simu ya Airtel ya kujenga mnara wa simu katika Kata ya Mwamagembe:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (K.n.y NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa huduma ya mawasiliano rasmi katika maeneo yote nchini, kwanza, kwa ajili ya kupeana taarifa na pia katika kufanikisha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, kutokana na dhamira ya dhati kuhakikisha kuwa maeneo yote nchini yanafanikiwa na huduma za mawasiliano Serikali imeendelea kuhakikisha makampuni ya simu za mkononi yanapeleka mawasiliano ya simu na mara kwa mara kampuni hizo zimekuwa hivyo kulingana na mipango yake na bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake, Kampuni ya Simu ya *Airtel* ilifanya utafiti wa masoko katika eneo la Kata la Mwamagembe na kuliweka katika eneo hilo katika orodha ya maeneo ambayo yangeweza kuwekewa minara kufikishiwa huduma ya mawasiliano katika mwaka huu wa fedha 2012/2013. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kibiashara na mipango ya uwekezaji ya mwaka huu, kampuni hiyo imeahidi kuliweka eneo la Kata ya

Mwamagembe kwenye mipango yake ya uwekezaji kwa mwaka ujao wa fedha ili kuweza kujenga mnara wa simu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo, ni mwaka wa tatu sasa toka hii kampuni ilipofanya utafiti na kutoa ahadi ya kuja kuweka mnara pale Mwamageni na mbaya zaidi wenzao wa *VODACOM* waliweka mnara Mgandu. Halafu wakaendelea wakaruka pale Mwamagembe wakaweka Rungwa na kuwaacha wananchi wa Mwamagembe bila mawasiliano yoyote kwa sababu ya ahadi hii ya hii Kampuni ya *Airtel*.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi suala hili sasa limechukua sura ya kisiasa kwa sababu inaonekana kama vile tunatoa ahadi hewa. Sasa ningependa kumwomba Waziri au kumuuliza Waziri anaweza akafunga safari mara baada ya kikao hiki ili twende Mwamagembe ikiwezekana na Afisa wa *Airtel* kwenda kuwahakikishia wananchi juu ya ahadi hii mpya?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri amesema mwaka wa fedha ujao, lakini ninavyofahamu mwaka wa fedha wa Serikali unatofautiana na miaka ya fedha ya haya makampuni, je, ni lini hasa mwaka wa fedha kwa maana ya mwaka wa fedha wa hii kampuni ya *Airtel*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema kwamba, kweli makampuni yamekuwa yakiahidi, lakini ni vyema vile vile Mbunge akatambua kwamba kutokana na mabadiliko ya kibiashara

ahadi hizo zinabadilika mara kwa mara. Lakini nimhakikishie tu kwamba, pamoja na Makampuni haya ya Simu, Serikali kupitia Mfuko wa *UCAF,* tayari imeshatangaza tenda kwa ajili ya Kata 152 ili kuhakikisha kwamba, mawasiliano yanafika katika maeneo kama hayo. Kuhusu miaka ya fedha ya makampuni haya ni kweli yanatofautiana na mwaka wa fedha wa Kampuni ya *Airtel* unaoanza tarehe 1 Aprili. Kwa hiyo, ni kuanzia tarehe 1 Aprili, 2013.

Na. 12

**Kusambaza Majiko Madogo na Mitungi ya Gesi**

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA – (K.n.y. MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA)** aliuliza:-

Serikali imedhamiria kukamilisha ufungaji wa bomba la gesi asili kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na hivyo kupunguza gharama ya gesi kwa matumizi ya majumbani na kuepuka matumizi ya mkaa yanayosababisha uharibifu wa mazingira.

Je, Serikali ina mipango gani ya kupeleka majiko madogo na mitungi ya gesi katika mikoa ambayo bomba hilo la gesi litapita?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI – MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba rasilimali ya gesi asili inachangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu Serikali inaandaa mikakati mbalimbali ya kuhamasisha na kujenga mazingira yatakayowezesha kuongezeka kwa matumizi ya gesi asili katika shughuli mbalimbali za maendeleo kwa wananchi wote.

Mikakati hiyo ni pamoja na kujenga miundombinu kwa ajili ya kufikisha gesi asili katika sehemu mbalimbali nchini. Aidha, Serikali katika kuwezesha upatikanaji wa mitambo na vifaa vya kujenga miundombinu ya gesi asili imetoa msamaha wa kodi kwa baadhi ya vifaa kutumika kwa ajili ya gesi asili iliyoshindiliwa na gesi asili ya mabomba na vifaa vitakavyotumia katika mitambo ya kusindikia gesi asili kabla ya kuingiza kwenye bomba.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vifaa vilivyotolewa msamaha ya kodi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati wa mawasilisho ya bajeti ya mwaka 2012/2013 ni pamoja na vifaa vinavyoongezewa kwenye magari ili yaweze kutumia gesi asili, mitungi maalum ya kutumia gesi asili iliyoshindiliwa, vifaa vidogo vidogo vinavyotumika katika ujenzi wa mabomba ya gesi asili katika mitambo ya kusindikia gesi asilia.

Aidha Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya *Petrol* Tanzania *TPDC*, inatekeleza mradi wa mfano kwa ajili ya usambazaji wa gesi asili majumbani ikianzia katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba siyo tu majiko na mitungi midogo inapatikana

kwenye mikoa ambayo bomba linapita, bali kuhakikisha kwamba mikoa yote na hasa vijiji, majiko na mitungi ya bei nafuu inapatikana mahali popote kwa kushirikiana na sekta binafsi.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ambayo hayakuridhisha, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili. Kwa kuwa Serikali ina sera mahususi ya kulinda viwanda vyake nchini na rasilimali zake kama zinavyofanya nchi nyingine; na kwa kuwa moja katika rasilimali ya Tanzania ni gesi; na kwa kuwa kwa taarifa nilizonazo *TPDC*, imeomba shilingi bilioni 50 kwa ajili ya mradi wa kukandamiza gesi, bila mafanikio hadi leo; na kwa kuwa Serikali hii kuna gesi inaagizwa kutoka nchi za nje inatumika kwa kupikia:-

Je, Serikali ina mpango gani kuifanya gesi iwe rahisi na kuondoa matumizi ya mkaa kwa ajili ya kulinda uharibifu wa mazingira? Pia je, ni kwa nini Serikali mpaka hivi leo inaagiza gesi ya kupikia wakati gesi tunayo nchini badala ya kuiwezesha *TPDC* kuendeleza mtambo huu wa kukandamiza gesi? Kwa nini Serikali haijaifanya hivyo katika hiyo miundombinu inayofanya?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili …

**SPIKA:** Swali, siyo hotuba.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Naam.

**SPIKA:** Pili, liwe swali.

**MBUNGE FULANI:** Siyo hotuba.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Swali la pili, hadi hivi leo gesi ni suala la Muungano, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweza kupata fedha kama mkopo, kama ni namna yoyote ya kuwezesha kujenga bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam. Je, kuna mpango gani wa kupata fedha vile vile kujenga bomba la gesi kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar ili Zanzibar inufaike na gesi ili tusione hii Jamhuri ya Muungano inapendelea upande mmoja tu na kuidhalilisha Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwamba sera ya kulinda rasilimali zetu ikiwa ni pamoja na gesi, *TPDC* wameomba fedha na fedha hizo hawajapata kwa ajili ya kutengeneza bomba la gesi. Hapa ameuliza maswali mengi kidogo kwa pamoja, lakini nataka kusema tu kwamba *TPDC* kwa sasa wanatekeleza mradi ule wa Dar es Salaam wa usambazaji wa gesi ili tuweze kutumia gesi majumbani.

Kwa hiyo, fedha zote hizo zimetolewa na Serikali na kwa awamu kadri uwezo utakavyoruhusu na ndiyo dhamira ya Serikali kama nilivyosema kwamba, ni kuhakikisha tunaweza kufanya hivyo, siyo kwa eneo moja bali ni kwa nchi nzima. Lakini kwamba gesi tunayo ni jambo zuri, ni kweli tunayo, lakini hatujafikia kwenye hatua ya uzalishaji, tumegundua gesi inayotoka ile Msimbati inazalisha umeme unaotumika kwenye mikoa miwili ya Mtwara na Lindi, lakini gesi inayotoka Songosongo ndiyo inayozalisha umeme Dar es Salaam na baadhi ya viwanda bado tuna gesi kidogo ambayo tunaizalisha sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini hiyo tuliyoigundua hatujafikia kiwango cha kuanza kufanya *production,* kwa hiyo tusubiri wakati huo ukifika tutafikia kwenye hatua hiyo, kwani swali la msingi lilikuwa linataka tu maandalizi gani yanafanyika katika kukabiliana na suala zima la matumizi ya gesi ya majumbani.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, gesi ni suala la Muungano, lakini kama ilivyo katika gesi, basi tufikirie pia katika mafuta kwamba, nalo pia liwe ni suala la Muungano na kwamba baadaye tunakoendelea kama nilivyosema, basi tutaangalia hata uwezekano huo kwa sababu mambo haya yote ni mambo ya Muungano. Ahsante sana.

Na. 13

**Kutofautiana kwa Vivutio vya Uwekezaji Nchi za Afrika Mashariki**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Vivutio vya uwekezaji vinatofautiana miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na ushindani usio na haki kati yake na nchi nyingine wanachama?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutambua changamoto iliyopo na kutofautiana katika utoaji wa vivutio vya uwekezaji yaani *investment incentives*, tayari zimeanza mchakato wa kuoanisha vituo hivyo yaani *Investment Promotion Centre,* lakini pia na vivutio vinavyotolewa na vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nchi wanachama pia zimeona huu mfumo na utaratibu maalum ambao wanaitwa *EAC Model Investment Code* ambao utaziongoza nchi wanachama katika utoaji wa vivutio na uwekezaji vinavyowiana. Aidha, nchi wanachama zimejitengenezea mikakati ya pamoja katika kutangaza vivutio vya kuhamasisha wawekezaji kutoka nje yaani *EAC Joint Export and Investment Promotion Strategies* na uendelezaji wa sekta binafsi yaani *EAC Investment and Private Sector Promotion Strategy*.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuhakikisha kunakuwepo na ushindani wa haki katika masoko ya bidhaa mbalimbali nchi wanachama vimeanzisha na sheria mbalimbali kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Ushindani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2006;

(b) Sheria ya Kusimamia Viwango, Ubora na Vipimo Sahihi vya Bidhaa ya Mwaka 2006 *EAC Standardization, Quality Assurance, Meteorology and Testing Act;*

(c) Kanuni na taratibu za Ushindani za mwaka 2010; na

(d) Kuundwa kwa Mamlaka ya Ushindani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *EAC Competition Authority* ambayo majadiliano yake bado yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali kwa kupitia Tume ya Ushindani ya Tanzania *(Fair Competition Commission)* chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara inaendelea kusimamia ushindani wa haki katika kufanya biashara nchini.

**MHE. MARGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa, nina maswali mawili madogo ya kuuliza. Kwanza, vyombo hivi vilivyoweka naamini vinashughulika kutatua matatizo ya vikwazo vya kiforodha, je, Serikali inafahamu kwamba mpaka sasa hivi vimezuka na vikwazo vingi visivyo vya kiforodha ambapo wafanyabiashara wetu kutoka Tanzania wakienda nchi jirani wanapata vikwazo vya kupeleka bidhaa zao?

Swali la pili, kama Serikali inafahamu vikwazo hivyo na naomba hasa itueleze ili watu wasibabaishwe inachukua hatua gani ili kukabiliana na vikwazo hivyo ambavyo siyo vya kiforodha?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba na ni lazima nikiri kuna vikwazo vingi sana vya kiforodha na nchi wanachama, lakini kabla sijaendelea kuzungumzia hilo, lazima nitoe taarifa kwa Bunge Tukufu na wananchi kwamba mkataba wa Afrika Mashariki pamoja na *Protocol* ya umoja wa

forodha unahalalisha kuweko kwa *fair competition* katika nchi wanachama. Kuna *Article* namba 21 ya *Customs Union* na *Treat* yenyewe kwenye *Article* namba 75 inazungumza hivyo kwamba *competition* kwanza ipo, hilo lazima likubalike.

Mheshimiwa Spika, lakini vikwazo vile vile vinatoka na zile nchi jinsi zinavyokaa na kutazama namna gani tunaweza kupata mapato. Lakini jibu kwa kifupi tu ni kwamba, nchi zimeshakaa kikao na Mawaziri wamekaa kitako katika sekta tofauti na vikwazo vinapunguzwa na vilikuwa ni vingi sana na ikifika Desemba, 2012 tutahakikisha kwamba vikwazo vingi sana vimeshapunguzwa miongoni mwao, kwa mfano, vikwazo vya mauzo ya chai, kuna vikwazo vya bidhaa za magari, vikwazo vile vya usafiri kutoka bandarini na kuna nchi nyingine upimaji wa mizani za uzito.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa ufupi natoa taarifa hii kwenu nyie Bunge Tukufu na ikiwezekana kuna jedwali kubwa sana nitalipatia hili Bunge lako na Waheshimiwa Wabunge ili uweze kujua kwamba Wizara yetu pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki imepunguza vikwazo gani na kufikia Desemba, 2012 vikwazo gani vitakuwa vimekamilika.

Na. 14

**Fidia kwa Wananchi Waliohamishwa Kupisha Reli**

**MHE. OMAR R. NUNDU** aliuliza:-

Wakazi wa sehemu ya Magaoni, Kata ya Mabawa na Tangasisi Jijini Tanga walishataarifiwa kuwa watahamishwa katika maneo yao ili kupisha ujenzi wa Reli mpya na kwamba tathmini ya fidia yao itafanywa na ifikapo mwezi Aprili, 2012 wangekuwa wamelipwa, suala ambalo halijatekelezwa hadi sasa.

Je, Serikali inasema nini kuhusu hatma ya wananchi hao takribani 650 juu ya makazi yao na ulipwaji wa fidia?

**WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini kama ifuatavyo:-

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia *RAHCO* iliwasiliana na Manispaa ya Tanga na kukubaliana na kutenga ekari 150 katika eneo la Mwambani kwa ajili ya kujenga sehemu ya kupanga mabehewa *(Marshalling yard).* Katika kutekeleza suala hilo, *RAHCO* imeweka Mshauri Mwelekezi M/S *Majengo Estates Developer Limited* kwa ajili ya kufanya tathmini ya fidia kwa wananchi wa maeneo hayo. Taarifa iliyowasilishwa na Mshauri Mwelekezi inaonesha kwamba gharama na fidia za wakazi wa Magaoni ni shilingi bilioni 5.3.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, nyaraka za fidia zipo Manispaa ya Tanga kwa ajili ya uhakiki wa umiliki wa ardhi na makazi kwa wananchi hao katika ngazi ya Kijiji, Wilaya na Mkoa, uhakiki ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2012. Baada ya zoezi hilo kukamilika,

hundi zitaandaliwa kwa ajili ya kufanya malipo ya fidia kwa wananchi hao.

**MHE. OMAR R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri yanayowatia matumaini wakazi wa Magaoni, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la malipo ya wakazi wa Magaoni ni la muda mrefu na huko nyuma walishaahidiwa kwamba, wangelipwa mwezi Mei mwaka huu na katika hotuba ya bajeti, Waziri aliahidi kwamba, wangelipwa mwezi Septemba. Sasa tunaona kunakwenda taratibu za uhakiki zinazoashiria mwezi huu wa Oktoba, inaweza ikachelewa tena. Je, inapotokea malipo yakichelewa sana, wananchi hawa huwa wanafidiwaje kutokana na usumbufu kutokana na kutokuendeleza miradi yao ya maendeleo kwa ucheleweshaji kama huo?

Pili, Serikali kwa nia njema kabisa inajitahidi kushika sehemu nyingi kwa shughuli mbalimbali na sehemu hizo zinatokana na wananchi, kuna la Reli na pia *EPZ*. Serikali ina mikakati gani ya uhakika pamoja na kutathmini upya sehemu hizo zinazoshikwa kuhakikisha kuwa sehemu zinazoshikwa wananchi wanalipwa kwa wakati na kazi zinazotakiwa kufanywa pale zinafanywa kwa wakati ili kuondoa usumbufu na ulalamikaji na pia hasara za kimaisha kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, ahsante!

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la swali la msingi, ni kwamba, kwa upande wa Serikali, tayari tunayo fedha ya fidia, lakini ni lazima tufuate taratibu za malipo yaani ni lazima tathmini ifanyike, ni lazima uhakiki wa hiyo tathmini ufanyike na ndiyo kitu ambacho tunakisuburi. Nyaraka za fidia kama nilivyosema zipo Manispaa ya Tanga kwa uhakiki.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge basi atumie nafasi yake ya Ubunge kuusukuma uhakiki ukamilike haraka ili sisi tuweze kutekeleza hayo malipo, pesa tunayo.

Mheshimiwa Spika, ningependa nimalizie kwa kusema kwamba, Serikali inapochukua maeneo haya inakuwa na uhakika kwa asilimia mia moja kwa kitu ambacho itakifanya kama ambavyo tutafanya katika eneo hilo la Tanga.

**SPIKA:** Ahsante! Mheshimiwa Mbilinyi!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa kuniona. Nataka kumuuliza kaka yangu Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe kwamba kuboresha reli ni pamoja na kuboresha mazingira ya kibiashara kwa hizo reli. Katika hili Mbeya tuna *project* ya *Dry Port* Iyunga ambayo itakapoanza kazi itasaidia sana kutoa biashara kwa Reli ya *TAZARA* na kinachotukwamisha kutoka Serikalini ni leseni tu kwa ajili ya kituo kile ili kibadilike na kuwa *Mbeya Dry Port* kitu ambacho wao kama *Management* wameshafanya maandalizi yote.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kupata kauli ya Waziri au ya Serikali kwamba, ni lini hasa Serikali itatoa leseni kwa

*Mbeya Dry Port* Iyunga ili ianze kazi na kutoa ajira pamoja na kutoa biashara kwa *TAZARA*.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, maombi ya kuanzisha *Dry Port* tumepokea mengi siyo tu la Iyunga, lakini kwa Mkoa wa Mbeya huo huo kuna maeneo zaidi ya matatu, Serikali inayafanyia kazi na tutampa majibu muda muafaka utakapowadia.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umepita. Lakini pamoja na kwamba tulianza na shughuli nyingine wakati tunaanza Bunge, lakini nilichojifunza hapa ni kwamba, mmesahau kwani maswali yenu ya nyongeza ni marefu yanakuwa hotuba.

Kwa hiyo, yanatufanya tusiwe na maswali mengi ya nyongeza mengine kwa wengine maana unakuta mtu mmoja anauliza kwa dakika tano. Sasa wewe peke yako unauliza dakika tano! Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba turudie tabia ya zamani, maswali ya nyongeza yanatakiwa yawe mafupi ili Wabunge wengi wapewe nafasi, siyo kuwahutubia wengine na Mawaziri pia mjaribu kupunguza urefu wa majibu.

Tuna matangazo ya kazi; Mheshimiwa James Lembeli ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, watakuwa na kikao na nimewaruhusu kufanya leo saa nne asubuhi katika Ukumbi namba 219, Jengo la Utawala, nimewaruhusu wafanye hivi kwa sababu nahitaji wakamilishe kazi yao mapema ili iingie kwenye ratiba.

Pia, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margareth Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, watakuwa na kikao leo saa saba mchana, katika Ukumbi namba 227, Jengo la Utawala. Muda huo tutakuwa na *briefing,* kwa hiyo, Mwenyekiti nadhani utaangalia namna ya kufanya.

Lakini pia nina tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Idd Azzan kwamba, taarifa kuhusu michezo wakati wa Mkutano wa Tisa wa Bunge ambao umeanza leo mpaka tarehe 9/11/2012, wanamichezo wote wanaarifiwa kuwa mazoezi ya viungo na ya michezo mbalimbali yataendelea kwenye viwanja husika. Uwanja wa Jamhuri kwa mpira wa miguu, mbio, mazoezi ya viungo na *netball* na *CBE* mpira wa kikapu yaani *basketball*.

Jumamosi tarehe 3/11/2012 kutakuwa na mchezo wa kirafiki wa mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club* na *Mburahati Queens*, timu ya wanawake wakiungana na Jukwaa la Katiba Tanzania ili kuhamasisha Watanzania kushiriki maoni kuhusu Katiba mpya ya Tanzania. Wachezaji wote wahudhurie mazoezi kuanzia kesho asubuhi saa 12 katika uwanja wa Jamhuri.

Pia tarehe 3/11/2012 tutakuwa na ile Tume ya Maoni ya Katiba sisi Wabunge, sijui ndiyo wameunganisha hapo, basi tena ndiyo itakavyokuwa.

Lakini Waheshimiwa Wabunge pia tuna tangazo la msiba, Mheshimiwa John M. Cheyo amefiwa na mtoto wake *Belinde Hotel Dar es Salaam* kwa kuzama katika maji.

Kwa hiyo, maiti imepelekwa Shinyanga kwa maziko, hii ni taarifa ambayo tumepewa kwamba, kijana wake huyo alikwenda kuogelea basi akazama maji. Basi, tumwombee roho yake iweze kupumzika mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea! Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano Kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya Pamoja na Nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific *(Cotonou Agreement Partnership)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Azimio hili ni marekebisho ya pili ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya na nchi za Afrika, Caribbean na Pacific.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Azimio la kuridhia marekebisho ya pili ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya na Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific yaani *Second Amendment to the Partnership Agreement between the European Community and the Member States of African, Caribbean and the Pacific* kwa kifupi inaitwa *ACP Group.*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Fedha na Uchumi

chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi kwa kujadili kwa kina Azimio hili na kutoa ushauri thabiti uliosaidia kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Azimio hili limezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazonufaika kupitia ushirikiano chini ya mkataba ujulikanao kama *The Cotonou Partnership Agreement* kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya na nchi za *ACP*. Mkataba huu ulisainiwa mnamo tarehe 23 Juni, 2000 mjini *Cotonou,* Benin na wawakilishi wa nchi zote 77 za *ACP* ikiwepo Tanzania na nchi 25 za Jumuiya ya Ulaya yaani *European Union* wakati huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa sasa Umoja huu una jumla ya nchi wanachama 78 baada ya kujumlisha nchi ya Sudani ya Kusini kujiunga na *ACP*. Mkataba huu uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Azimio lake namba nne la tarehe 10 Agosti, 2001 na utekelezaji kwa kipindi cha miaka 20 ndiyo muda wake kuanzia mwaka 2001 mpaka 2020 katika awamu nne za miaka mitano mitano.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya *Cotton Wool Partnership Agreement* ni kujenga ushirikiano imara na dhabiti utakaowezesha kujenga uchumi endelevu ili kupunguza na hatimaye kuondoa umaskini katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha malengo haya, maeneo matatu ya ushirikiano yameainishwa. Kwanza, ni Ushirikiano wa Kimaendeleo na Kifedha (*Development and Financial Cooperation).* Pili, Ushirikiano wa Biashara na Vitega Uchumi (*Trade and Investment)* na tatu ni majadiliano ya Kisiasa yaani *Political Dialogue.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 95(3) cha Mkataba huu, nchi wanachama zinaweza kufanyia marekebisho Mkataba huu kila baada ya miaka mitano endapo kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mkataba huu sasa ulifanyiwa marekebisho ya kwanza mjini *Luxembourg* tarehe 25 Juni, 2005 ambapo Tanzania iliridhia kupitia Azimio la Bunge namba 10 la mwaka 2006. Majadiliano ya marekebisho ya pili yalihitimishwa tarehe 22 Juni, 2010 Mjini Ouagadougou, Burkina Faso. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini marekebisho hayo tarehe 29 Oktoba, 2010.

Mheshimiwa Spika, faida ya kuridhia Mkataba huu wa Ushirikiano wa *Cotonou*. Tangu utekelezaji wa Mkataba huu uanzie mwaka 2001 hadi sasa Tanzania imenufaika katika maeneo mbalimbali kama nitakavyoeleza hapa chini.

Kwanza, tumenufaika na mikopo ya masharti nafuu kutoka Benki ya Rasilimali ya Ulaya (*European Investment Bank)* kwa ufadhili wa miradi ya *program* mbalimbali za maendeleo hususan kugharamia mradi wa kujenga gridi ya umeme, kuunganisha Mikoa ya Iringa na Shinyanga, tulifanikiwa kupata *Euro* milioni 134.5 na upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora,

Bukoba, Shinyanga na Sumbawanga ambapo tulifanikiwa kupata *Euro* milioni 50.

Pili, tulifanikiwa kupata msaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya kwenye maeneo ambayo yalifadhiliwa na mpango wa Tisa wa Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya yaani *European Development Fund* namba tisa, iliyotekelezwa mwaka 2001 mpaka 2007. Tanzania imenufaika kwa kiasi kikubwa kupitia utaratibu wa biashara wa Bahasha A na Bahasha B kama ifuatavyo:-

Kundi la kwanza yaani *Envelope A* tulipata jumla ya *Euro* milioni 509 kama ifuatavyo:-

*Program* ya kuchangia katika bajeti kuu ya Serikali yaani *General Budget Support* kwa ajili ya kugharamia sekta za mikakati na *program* za kukuza uchumi na kupunguza umaskini tulifanikiwa kupata kiasi cha *Euro* milioni 150;

Pili, tulifanikiwa kupata Euro milioni 43.5 zilizotolewa kusaidia utekelezaji wa *program* za sekta ya elimu;

Tatu, tulifanikiwa kwa ajili ya miradi ya miundombinu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Bandari ya Zanzibar ambapo pale tulifanikiwa kupata *Euro* milioni 42. Vile vile barabara za Isaka – Tinde – Nzega tulipata *Euro* milioni 114. Vile vile barabara ya Morogoro hadi Dodoma tulipata Euro milioni 42, barabara za Jiji la Mwanza tulipata Euro milioni 29 na barabara ya Mandela, Jijijni Dar es Salaam tulipata Euro milioni 32;

Nne, tulipata *Euro* milioni 3.8 zilizotolewa kusaidia Asasi Zisizo za Kiserikali; na

Tano, tulipata *Euro* milioni 22.7 zilizotolewa katika sekta ya utawala bora uliolenga kujenga uwezo wa utawala na uongozi katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kundi la pili yaani Bahasha B tulipata jumla ya *Euro* milioni 66.2 kwa mpangilio ufuatao:-

Kwanza, kati ya fedha hizo, Euro milioni 6.5 zilitolewa kuchangia Mfuko wa kulinda amani katika nchi za Afrika ambapo Tanzania mwanachama; na

Pili, kiasi cha *Euro* milioni 59.7 kilihamishwa kutoka Bahasha B kwenda Bahasha A ili kuongeza fedha za utekelezaji katika maeneo yaliyoainishwa hapo juu;

Mheshimiwa Spika, msaada tuliopewa upande wa *program* ya *STABEX*. Kiasi cha *Euro* milioni 44 kilitolewa kwa ajili ya Mfuko wa *STABEX* kwa ajili ya kugharamia yafuatayo:-

(i) utafiti wa zao la Kahawa ambapo tulinufaika kupata *Euro* milioni 13.5;

(ii) Sekta ya Kilimo yaani *ASDP* tulifanikiwa kupata *Euro* milioni 18;

(iii) Ujenzi wa ukarabati wa barabara za vijijini kwa mikoa inayolima zao la kahawa, tulifanikiwa kupata *Euro* milioni 12 ambapo jumla ya barabara zenye urefu wa kilomita 635.3 zilijengwa na kukarabatiwa katika Mikoa ya

Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Ruvuma, Kagera, Mara, Kigoma na Mkoa wa Mbeya; na

(iv) Ilikuwa ni uratibu na ufuatiliaji ambapo katika shughuli hii tulifanikiwa kupata *Euro* 0.9 milioni.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2008 mpaka 2013 misaada kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya imeelekezwa kwenye maeneo ambayo Tanzania ilishiriki katika kuyaanisha katika mpango wa 10 wa Mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya ya Ulaya (*European Development Fund, 10).*

Mheshimiwa Spika, kiasi cha *Euro* 670.05 milioni kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza *program* na miradi iliyoainishwa katika Bahasha A na B kama ninavyoeleza hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, katika kundi A yaani Bahasha A ni *Euro* milioni 606.51, kiasi cha *Euro* milioni 505 zimetengwa kwa ajili ya misaada ya kibajeti yaani *General Budget Support* kugharamia utekelezaji, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (*MKUKUTA)* na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA*)*.

Mheshimiwa Spika, pili, kiasi cha *Euro* milioni 139 kimetengwa kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi ya miundombinu hususan usafirishaji kupitia Mpango wa Kusaidia Bajeti za Kisekta (*Transport Sector Budget Support)*.

Mheshimiwa Spika, tatu, kiasi cha *Euro* milioni 55.5 zimetengwa kwa ajili ya kusaidia masuala ya kuimarisha

barabara na mtandao wa Kikanda (*Trade and Regional Integration)*.

Mheshimiwa Spika, nne, kiasi cha *Euro* milioni 51.51 kimetengwa kwa ajili ya kusaidia kufikiwa kwa Malengo ya Milenia kwenye sekta ya maji ambapo miji ya Lindi, Sumbawanga na Kigoma itanufaika.

Mheshimiwa Spika, tano, asasi zisizo za Serikali zimetengewa Euro milioni 23 na kati ya fedha hizo kiasi cha Euro milioni 10 zimetengwa kusaidia Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira, *Euro* milioni 10 zimetengwa kusaidia Uendelezaji wa Utamaduni na *Euro* milioni tatu (3) zimetolewa kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kuboresha na kuimarisha demokrasia ya utawala bora, kujenga uwezo wa asasi za kiraia katika masuala ya uwajibikaji na ushiriki wake katika sera na mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sita, ni Programu ya Maboresho ya Sekta ya Umma ambayo imetengewa *Euro* milioni nane. Hii inajumuisha Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, saba, misaada ya kiufundi imetengewa *Euro* milioni tano.

Mheshimiwa Spika, nane, miradi ya Nishati ya Umeme imetengewa *Euro* milioni nane. Miradi hiyo ni kama hii ifuatayo:-

(i) *Sustainable Community based hydropower supply in six villages in* Ludewa *District;*

(ii) *Access to modern energy services in Nkondo Ward.* Hii iko katika Wilaya ya Njombe;

(iii) *Cluster Solar PV projects* ambayo iko katika *Lake Zone;*

(iv) *Introducing a new concept for affordable biogas system to connect ten thousands (10,000) rural households in Tanzania;* na

(v) *Iyovi hydropower project.* Hii iko Mikumi katika Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, tisa ni uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 ambapo zilitolewa Euro milioni tatu ambazo tulinufaika nazo kutokana na programu hii.

Mheshimiwa Spika, kumi, ni misaada ya kiufundi ambayo imetengewa *Euro* milioni tano.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja ni uratibu na ufuatiliaji ambapo tumepewa *Euro* milioni tano.

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili ni fedha za dharura ambapo zilitengwa *Euro* milioni 3.5 na Euro milioni 3.1 tayari zimeishatolewa kusaidia ile Bandari ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kundi B, *Euro* milioni 63.54 zimetengwa kugharamia miradi inayolenga kushughulikia madhara yatokanayo na majanga ya asili na kulinda amani katika nchi za Afrika ikiwemo Tanzania, kama ifuatavyo:-

(i) Kiasi cha *Euro* milioni 6.6 tayari kimeidhinishwa kutumika kwa ajili ya kurejesha makazi kwa wananchi wa Kilosa waliokumbwa na mafuriko kati ya mwaka 2010 na 2011;

(ii) Kiasi cha *Euro* milioni 20 kilitolewa mwezi Desemba, mwaka 2010 ikiwa ni msaada wa chakula *(food security)* kupitia bajeti kuu ya Serikali; na

(iii) Kiasi kilichobaki kitategemea mahitaji kama ilivyoanishwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme juu ya vifungu muhimu vya Mkataba vilivyofanyiwa marekebisho ya pili. Ili kufikia malengo yaliyotarajiwa ya ushirikiano baina ya nchi wanachama, marekebisho muhimu yafuatayo yamefanyika kwa lengo la kuboresha mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Kwanza ambayo imefanyiwa marekebisho ni katika aya ya 3 na 4 za mkataba ambapo nchi za Afrika, *Caribbean na Pacific* zimekubaliana kushirikiana kwa kuweka misimamo yao ya pamoja katika kufikia malengo ya Milenia na kwamba zitashirikiana kwa pamoja kutatua matatizo yao kwa kutilia maanani hali ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na mazingira katika maeneo yaliyofikiwa na nchi zenyewe. Aidha, nchi hizi zitatilia mkazo umuhimu wa kuisaidia sekta binafsi katika kuongeza fursa za ajira, upatakanaji wa haki kwa wananchi na kupata mahitaji ya lazima katika maisha.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya Pili imefanyiwa marekebisho vilevile kwa kuifuta na kuiandika upya ili

kuendeleza ushirikiano kati ya Umoja wa Ulaya na nchi za Afrika, *Caribbean* na *Pacific* kwa misingi ya kisheria na uwepo wa taasisi za pamoja. Aidha, ushirikiano huu utaendelea kusisitiza kuhusu mikakati ya kimaendeleo katika Serikali ya nchi husika, Mabunge, Serikali za Mitaa na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya kijamii kama vile sekta binafsi na asasi za kiraia.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 28 imefutwa na kuandikwa upya ili kusisitiza kwamba:-

Kwanza, ushirikiano baina ya *ACP* na *European Union* utatoa misaada yenye ufanisi ili kuweza kufikia malengo ya maeneo ya kipaumbele ambayo yameanishwa na nchi wanachama wa *ACP* na kwamba ushirikiano baina ya *ACP* na *European Union* una lengo la kusaidia upatikanaji wa amani na usalama, kuzuia migogoro na kutoa misaada au usuluhishi pale inapohitajika.

Pili, ushirikiano una lengo la kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi kwa njia ya kujenga masoko makubwa, kuruhusu uhuru wa kusafiri bila vikwazo kwa wananchi, kusafirisha bidhaa na huduma, upatikanaji mitaji, ajira na ubadilishanaji wa teknolojia baina ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, badiliko la nne, Ibara ya 29 imefutwa na kuandikwa upya ili kusudi kuweka wigo mpana wa ushirikiano wa Kikanda katika maeneo ya usalama na amani ili kuzuia migogoro.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huu utahusisha kuhimiza na kuhamasisha mazungumzo na majadiliano ya kisiasa

katika kuzuia na kutatua migogoro na haki za binadamu na demokrasia. Aidha, inasisitiza na kuhimiza jitihada za Kikanda katika ushirikiano wa masuala ya usalama hususani kuzuia silaha kuuzwa na kusafirishwa kiholela, dawa za kulevya, biashara ya fedha haramu, rushwa na uhalifu wa kupangwa.

Mheshimiwa Spika, katika nyanja ya uchumi, ushirikiano unalenga katika ushirikishwaji wa nchi zinazoendelea katika kuanzisha masoko ya Kikanda na kuhimiza maboresho katika sekta mbalimbali za kiuchumi na zile za kijamii na kuhimiza uwekezaji baina ya nchi na kuvutia vitega uchumi kutoka nje na ndani ya nchi zenyewe.

Mheshimiwa Spika, badiliko la tano, hili ni kuongeza Ibara mpya Na. 32A. Ibara hii inahusu masuala ya tabianchi. Kwa mara ya kwanza nchi za Umoja wa Ulaya na *ACP* zinatambua changamoto za kukabiliana na madhara na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa moja ya masuala ya kiushirikiano.

Mheshimiwa Spika, pande zote zimekubaliana kuongeza juhudi za namna ya kujumuisha masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi katika ushirikiano wao wa kimaendeleo na kusaidia juhudi za nchi za *ACP* katika kukabiliana na madhara yatokanayo na matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, badiliko la sita, hii ni Ibara ya 34 (2) –(4) zimefutwa na kuandikwa upya kwa makusudi ili kuweka bayana kwamba lengo kuu la ushirikiano wa kibiashara ni pamoja na kujenga uwezo wa nchi wanachama wa *ACP* kushiriki kikamilifu katika biashara za kimataifa. Katika kukamilisha hili, nchi wanachama wa *ACP* watawezeshwa

kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kisera kuhusu biashara za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, badiliko la saba, hili ni Ibara ya 36 ambayo imefutwa na kuandikwa upya kwa makusudi ya kusisitiza nchi wanachama kushirikiana katika kukamilisha ushirikiano mpya kwa mujibu wa matakwa ya Shirika la Biashara Duniani *(The New World Trade Organization Compatible Economic Partnership Agreements*). Kuondoa vikwazo vya biashara miongoni mwao ndiyo sababu yake kubwa.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huu una lengo la kuharakisha ushirikishwaji wa nchi wanachama wa *ACP* katika uchumi wa Dunia kwa kutumia kikamilifu ushirikiano wa Kikanda na biashara kwa nchi za Kusini *(South South Trade).*

Mheshimiwa Spika, badiliko la nane, hili ni Ibara ya 61 ambayo imefanyiwa marekebisho kwa kuifuta aya ya pili na kuandika upya kwa makusudi. Ibara hii inahusu misaada ya kibajeti katika kusaidia maboresho ya kisekta na uchumi mpana. Misaada ya aina hii itatolewa kwa kuzingatia mipango iliyopo ya kimkakati ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Aidha, misaada hii itatolewa kwa kuzingatia mifumo chanya ya sera za kiuchumi iliyofanyiwa tathmini na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, badiliko la tisa ni kuongeza Ibara mpya ya 72A. Ibara hii inahusu misaada ya kibinadamu na majanga. Misaada hii itatolewa kwa lengo la kuokoa maisha, kutoa misaada ya kibinadamu, kuchukua hatua za muda mfupi kutengeneza na kujenga mifumo ya kiuchumi

kwa kutathmini mahitaji ya watu wasio na makazi maalum hususani wale wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha Azimio husika kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** kwa mara ya kwanza Tanzania iliingia Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya pamoja na nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific *(The Cotonou Partnership Agreement)* mwaka 2000 utakaodumu kwa kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2001 mpaka mwaka 2020;

**NA KWA KUWA** kwa mujibu wa kifungu cha 95 (3) cha Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya pamoja na Nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific, nchi wanachama wanaweza kufanya marekebisho kila baada ya miaka mitano, Mkataba huu ulifanyiwa marekebisho ya kwanza mwezi Juni, 2005 na kuridhiwa na Azimio la Bunge Na. 10 la mwaka 2006;

Mheshimiwa Spika, aidha, Mkatabaa huu umefanyiwa marekebisho ya pili yajulikanayo kama, *The Second Amendment to the Partnership Agreement between the European Community and the Member States of the African, Caribbean and Pacific Group (ACP).*

**NA KWA KUWA** Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazonufaika na misaada na mikopo kutoka Jumuiya ya Nchi za Ulaya, chini ya Mkataba huu;

**NA KWA KUWA** Mkataba huu uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Azimio Na. 4 la mwaka 2001;

**NA KWA KUWA** marekebisho ya pili yalifanyika mwezi Juni, 2010 na kusainiwa na Wawakilishi wa nchi zote 77 Wanachama wa Afrika, Caribbean na Pacific *(ACP)* ikiwepo Tanzania;

**NA KWA KUWA** kwa mujibu wa masharti ya Mkataba huu marekebisho haya yatakubalika na kuanza kufanya kazi baada ya theluthi mbili ($^2/_3$) ya nchi za *ACP* na *European Union* kuridhia;

**NA KWA KUWA** marekebisho ya Mkataba yataendelea kufaidisha Tanzania kwa kuweka misimamo ya pamoja katika kufikia malengo ya Milenia, kuweka wigo mpana wa ushirikiano wa Kikanda katika maeneo ya usalama na amani na kuzuia migogoro, kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi, kuondoa vikwazo vya biashara miongoni mwa nchi wanachama, kupata misaada ya kibajeti ya kusaidia maboresho ya sekta ya uchumi mpana na misaada ya kibinadamu na majanga ambayo itatolewa kwa lengo la kuokoa maisha na kutengeneza na kujenga mifumo ya kiuchumi kwa kutathmini mahitaji ya watu waliotawanyika hususan wakimbizi;

**KWA HIYO BASI** kwa kuzingatia manufaa yatakayotokana na marekebisho ya Mkataba huu kwa Tanzania na Wanachama wa nchi za Afrika, Caribbean na Pacific na nchi nyingine zinazoendelea na pia umuhimu wa

kukubali kufanya marekebisho ya Mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wa Tisa na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 liazimie kwamba:-

(a) Marekebisho ya Mkataba uitwao *Cotonou Partnership Agreement* kati ya nchi Wanachama wa Afrika, Caribbean na Pacific na Jumuiya ya Nchi za Ulaya yaridhiwe ili Tanzania iweze kushiriki katika kutekeleza makubalino ya Cotonou kwa mujibu wa marekebisho haya na kuiwezesha Tanzania kunufaika na hivyo kujenga uchumi endelevu ili kupunguza na kuondoa umaskini; na

(b) Wizara ya Fedha iendelee kusimamia kwa karibu zaidi sekta zote ambazo zinapata misaada na mikopo kupitia utaratibu huu ili Taifa liweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kutoa hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

**SPIKA:** Ahsante, hoja hii imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Azimio hili, Mheshimiwa Chenge au kwa niaba yake nani yule! Aah, Mheshimiwa Kitandula!

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha tumekutana tena katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Andrew John Chyenge, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007, niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya na Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific yaani *Second Amendment to the Cotonou Partnership Agreement between the European Community and the Member States of the African, Caribbean and Pacific Group.*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jumuiya ya Nchi za Ulaya ulianza mwaka 1975 wakati Tanzania, pamoja na nchi wanachama wengine wa Afrika, *Caribbean* na *Pacific (ACP)*, iliposaini Mkataba wa Kwanza wa Lome (*First Lome Convention*). Mikataba mingine mitatu *(LOME II-IV)* ilisainiwa baadaye kabla ya Mkataba wa sasa unaojulikana kama Ushirikiano wa Cotonou (*Cotonou Partnership Agreement*) uliosainiwa mwezi Juni mwaka 2000 na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Azimio Na. 4 la tarehe 10 Agosti, 2001. Mkataba wa Cotonou unalenga katika kujenga msingi mpya wa ushirikiano kati ya nchi 77 wanachama wa *ACP* na Jumuiya ya Ulaya (*ACP-EU Cooperation*) kwa kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2000 hadi 2020.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Mkataba huu ni kujenga ushirikiano imara na thabiti utakaowezesha kujenga uchumi endelevu ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa umaskini katika Nchi Wanachama pamoja

na kuiwezesha Tanzania kuendelea kunufaika katika nyanja zote za ushirikiano uliopo hivi sasa wa kimaendeleo na kifedha *(Development and Financial Co-operation)*; kibiashara na vitega uchumi *(Trade and Investment)*; na majadiliano ya kisiasa *(Political Dialogue).*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inakubaliana na Azimio hili lililowasilishwa na Waziri wa Fedha kwa kuwa tangu utekelezaji wa mkataba huu uanze mwaka 2000, Nchi yetu imenufaika katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Afrika, *Caribbean* na *Pacific*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Mkataba huu hufanyiwa marekebisho kila baada ya miaka mitano kwa mujibu wa Ibara ya 95 ya Mkataba husika, marekebisho ya kwanza yalifanyika tarehe 25 Juni 2005 ambapo Tanzania iliridhia mwaka 2006 kupitia Azimio la Bunge Na. 10/2006. Majadiliano ya marekebisho ya pili yalihitimishwa tarehe 22 Juni, 2010 mjini Ouagadougou ambapo Tanzania ilisaini marekebisho hayo tarehe 29/10/2010. Kwa mujibu wa Ibara ya 93 ya Mkataba huo Nchi Wanachama wanapaswa kuridhia marekebisho ya Mkataba ili kupata nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Spika, tangu utekelezaji wa Mkataba huu uanze mwaka 2000 hadi sasa, Tanzania imenufaika katika maeneo mbalimbali mfano:-

(a) Kupata mikopo ya masharti nafuu kutoka Benki ya Rasilimali ya Ulaya *(EIB)* kwa ajili ya ufadhili wa miradi na program mbalimbali hasa katika sekta ya miundombinu,elimu, utawala bora na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010;

(b) Misaada ya kibajeti *(General Budget Support)* pamoja na kugharamia utekelezaji wa MKUKUTA na MKUZA;

(c) Kupata misaada ya kifedha kwa ajili ya majanga ya asili na kulinda amani.

Mheshimiwa Spika, hii ni baadhi tu ya misaada ambayo nchi yetu imenufaika kwa kuwa mwanachama katika ushirikiano huu. Hivyo Kamati inaendelea kushauri Bunge kuridhia marekebisho ya Azimio hili ili kufikia malengo tarajiwa baina ya nchi wananchama.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano huu kati ya Umoja wa Ulaya na nchi za Afrika, Caribbean na Pacific unasisitiza kuhusu mikakati ya kimaendeleo sio tu na Serikali za nchi husika bali pia na Mabunge ya nchi zao. Kamati inatoa angalizo kuwa ni vema Bunge letu liwe linapata taarifa mbalimbali za majadiliano na mijadala mbalimbali inayohusu mikataba mbalimbali tuliyoridhia kutoka kwa Serikali pamoja na Wabunge ambao ni wawakilishi wetu. Hii itasaidia kuwa na ufahamu mkubwa wa hatua mbalimbali za kimaendeleo zinazofikiwa kwenye mikataba tunayoridhia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa Marekebisho haya ya Pili ya vipengele muhimu ya Mkataba huu yatasaidia kupiga hatua katika kufikia Malengo ya Millennia

pamoja na malengo tuliyojiwekea kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ikasimamia ipasavyo misaada ya kifedha inayotolewa kupitia mikataba hii ili kuhakikisha inatimiza malengo yaliyokusudiwa kwenye miradi ya maendeleo ya sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikiathirika na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa namna moja au nyingine yanachangia kuathiri hali ya uzalishaji wa mazao katika sekta ya kilimo inayotegemea mvua. Mabadiliko ya tabia nchi yatakuwa na athari kubwa kiuchumi hali ambayo itaongeza kiwango cha umaskini katika nchi mbalimbali Barani Afrika ikiwemo Tanzania. Kuridhiwa kwa Azimio hili kutatoa fursa kwa nchi za Umoja wa Ulaya na nchi za *ACP* ikiwemo Tanzania kutambua changamoto za kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi kama moja ya masuala yanayohusu ushirikiano na hivyo kuongeza juhudi za pamoja katika kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia nguzo kuu za ushirikiano kama zilivyoainishwa kwenye maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Fedha, Kamati inaona kuwa ni busara Bunge kuridhia Azimio hili kwa kuwa nchi itanufaika zaidi kiuchumi hasa katika Kupata fedha za kugharamia miradi ya maendeleo; Kukuza uchumi na kupunguza umasikini; Kuondoa vikwazo katika biashara kwa nchi wanachama wa *ACP*; Upatikanaji wa soko la uhakika kwa bidhaa na mazao yetu pamoja na Kuimarika kwa ushirikiano wa Kikanda katika kukuza amani na usalama; pamoja na uhakika wa upatikanaji wa chakula.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati walioshughulikia Azimio hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Oseler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Amour Abdulla, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Subira K. Mgalu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru, Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri Fedha na Watendaji Wakuu wa Wizara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa na kukamilisha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa ya Azimio hili.

Aidha, kipekee na sio mwisho wa kuwashukuru, naomba niwashukuru wananchi wa Mkinga kwa kunipa heshima hii ya kuwatumikia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS – (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha hotuba hii kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Zubeir Zitto Kabwe, kuhusu Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano Kati ya Jumuiya ya Nchi za Ulaya Pamoja na Nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki *[Cotonuo Partnership Agreement]* yaani *The Second Amendment to the Partnership Agreement Between The European Community and the Member State of the Afican, Caribbean and Pacific).* Imetolewa chini ya Kanuni ya 86(6), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jumuiya ya Nchi za Ulaya ulianza mwaka 1975 pale nchi yetu pamoja na nchi wanachama wengine wa Afrika, Caribbean na Pasifiki ziliposaini mkataba wa kwanza wa Lome na baadaye kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa sasa unaojulikana kama Ushirikiano wa Cotonuo uliosainiwa mwezi Juni, 2000 na kuridhiwa na Bunge letu mwezi Agosti, 2001.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kuwa madhumuni ya mkataba huu ni kujenga ushirikiano imara na thabiti unaowezesha kujenga uchumi endelevu ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa umaskini katika Nchi Wanachama. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa kujenga uchumi ulio imara ni kutokana na kuwa na sera nzuri, usimamizi na utekelezaji pamoja na mgawanyo unaokubalika kwa rasilimali za nchi. Lakini ushirikiano unaoelezwa katika Azimio hili, ni ushirikiano unaoendeleza unyonyaji kwa Mataifa yaliyoendelea dhidi ya yale yanayoendelea. Hadi hivi sasa hakuna ushahidi wowote wa Kisayansi unaonyesha kuwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika, Caribbean na Pasifiki zinafaidika na mahusiano yaliyopo kati yake na Wakoloni wa zamani kutoka nchi za Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Spika, katika kuonyesha kuwa ushirikiano huu unayanufaisha zaidi Mataifa ya Ulaya kuliko Mataifa ya Afrika, *Caribbean* na Pasifiki ni tabia ya Mataifa ya Ulaya kulazimisha ufunguzi wa masoko katika Mataifa yaliyoko katika ushirikiano kwa ajili ya Makampuni yanayotoka kwenye nchi zao. Aidha, mbali na masoko, Kandarasi kubwa zinazochukuliwa na Makampuni yao ya ushirikiano

wa namna hii, itakuwa ni vigumu sana kwa Mataifa ya Kiafrika kama Tanzania kuondoa umaskini kwani yanageuzwa kuwa masoko tu ya bidhaa kutoka nchi za Ulaya. Ushirikiano wetu huu unaifanya Tanzania iendelee kuwa mzalishaji wa malighafi na soko tu, lazima kubadilisha mahusiano ya namna hii kama tunataka uhuru wa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 34 kama inavyorekebishwa inaweka bayana kwamba lengo kuu la ushirikiano wa kibiashara ni pamoja na kujenga uwezo wa nchi wanachama wa *ACP* kushiriki kikamilifu katika biashara za Kimataifa. Katika kufanikisha hili, wanachama wa *ACP* watawezeshwa kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kisera kuhusu biashara za Kimataifa. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupatiwa maelezo zaidi pale Ibara inapoeleza kuhusu kujenga uwezo wa nchi wanachama kushiriki kikamilifu katika biashara za Kimataifa. Je, uwezo huo unajengwa kwa kuondoa au kulegeza vigezo kandamizi katika biashara vinavyosababisha nchi za *ACP* zisiweze kushiriki kikamilifu katika masoko ya Ulaya au uwezo unajengwa katika kuelewa jinsi wanavyotengeneza vigezo hivyo? Aidha, Ibara inaposema kuhusu nchi za *ACP* kuwezesha kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kisera kuhusu biashara za Kimataifa maana yake ni kushiriki kutengua sera zilizopo na kutengeneza mpya kulingana na hali halisi au ni kubariki sera zilizopo ili zionekane zinakubalika kwa nchi wanachama?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 36 inasisitiza Nchi Wanachama kushirikiana na kuhakikisha ukamilishaji wa ushirikiano mpya unaendelea na matakwa ya Shirika la Biashara la Dunia (*New Compartitable Economic*

*Partnership Agreements).* Ushirikiano huu una lengo la kuhakikisha ushirikishwaji wa Nchi Wanachama wa *ACP* katika uchumi wa dunia kwa kuwezesha ushirikiano wa ushirikishwaji wa nchi za Kusini *South South Cooperation.* Kambi ya Upinzani inaona kuwa dhamira hasa ya marekebisho sio kama yanavyotamkwa kwani *South South Cooperation* lengo lake kubwa lilikuwa ni kushirikiana na kubadilishana taaluma na wataalam, rasilimali na teknolojia miongoni mwa nchi zinazoendelea lakini kwa muktadha wa Ibara hii inaonyesha kuwa lengo kubwa si mabadilishano ya hayo mambo tajwa bali ni biashara zaidi na kama ni biashara ni dhahiri nchi za Ulaya zinahitaji soko la nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka Serikali ieleze Bunge imechukua tahadhari gani dhidi ya athari zilizotajwa na wadau kwa nyakati mbalimbali zinazoweza kusababishwa na uridhiwaji wa marekebisho hayo na mkataba wa uchumi wa ushirikiano wetu ambayo ni kama yafuatayo:-

(1) Kupungua kwa mapato kutokana na kodi ndogo za mapato ambapo tunapunguza kiasi cha fedha ambazo zingeweza kutumika katika miradi mingine ya maendeleo.

(2) Uzalishaji wa ndani kutoweza kuhimili ushindani wa bidhaa za vyakula vya kilimo zinazoingia kutoka katika Jumuiya ya Ulaya.

(3) Kupungua kwa uhuru wa Tanzania kutumia sera za kutoza ushuru kwa kanuni za soko katika kukuza upatikanaji wa vyakula muhimu vya ndani.

(4) Ubia wa uchumi hauzuii matumizi ya ya ruzuku kwa mazao ya kilimo, vyakula vinavyoingizwa kutoka Jumuiya ya Ulaya kwani wakulima wetu hawawezi kushindana kiuzalishaji na wakulima wa Ulaya wanaopatiwa ruzuku katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaliomba Bunge lako Tukufu kuwa Marekebisho haya ya Pili ya Mkataba wa Ushirikiano baina ya Nchi za Ulaya, Afrika, Caribbean na Pasifiki yaangaliwe na kujadiliwa kwa kina kabla ya kuridhiwa na Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa Tanzania imeshindwa kusaini makubaliano ya Ushirikiano wa Kibiashara wa Kikanda *(EPA)* na *EAC* na *EU* kutokana na kutokukubaliana kwa baadhi ya mambo. Sasa isije ukatumika ujanja ujanja wa Jumuiya ya Ulaya kwamba yale tuliyoyakataa katika majadiliano ya *EPA* yanaendelea kati ya *EAC-EU* yakaingizwa katika makubaliano ya *EU-ACP* kabla ya nchi wanachama wa *EAC* hatujakubaliana kusaini wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, moja ya misingi muhimu ya makubaliano katika Mkataba wa Cotonuo ni usawa kwa nchi wanachama katika umiliki na utekelezaji wa mikakati yao ya maendeleo. Ibara ya 61 ya marejeo ya pili yanayoridhiwa inahusu misaada ya kibajeti kusaidia marekebisho katika uchumi mpana. Nanukuu:-

*"Misaada ya aina hii itatolewa kwa kuzingatia kwamba mipango ya kimkakati ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini itatolewa kwa kuzingatia mifumo chanya ya sera za kichumi iliyofanyiwa tathmini na wadau wa maendeleo".*

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia marekebisho haya yanayotakiwa kuridhiwa katika Ibara hiyo, ni dhahiri kuwa nchi wanachama hasa zile zinazoendelea haziwezi kuendelea au kujikwamua kwa kuweka sera zao wenyewe na kwa kutumia rasilimali zao kwa kadri mazingira ya nchi zao yanavyoruhusu hadi wale wadau wa maendeleo wazihakiki kama kweli hazitakuwa na madhara kwa nchi zao, madhara yanayosemwa hapa ni uwezo wa kutokuhitaji soko la bidhaa au utaalamu wa aina yoyote toka Mataifa hayo ya Ulaya wakati sisi Mataifa yanayoendelea tuna uwezo wa kutengeneza bidhaa hizo na utaalamu husika. Aidha, kutathmini sera za nchi wanachama wa *ACP* na wadau wa maendeleo maana yake kwa tafsiri rahisi ni kwamba nchi za *ACP* hazina uwezo wa kutayarisha sera zake za uchumi kulingana na hali halisi za nchi zao au ni mkakati wa makusudi wa kupotosha sera zetu nzuri na kutulazimu kwenda upande wanaohitaji wao na kwa madhumuni waliyokwishayapanga. Hii sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kambi Rasmi ya Upinzani, kutokana na maelezo ambayo imeyatoa hapo juu inaona ni vyema uridhiaji wa Muswada huu uende sambamba na masharti au angalizo *(ratification with reservations)* kwani pamoja na manufaa ambayo Serikali imeyatoa bado tunaona manufaa hayo hayaoani na hasara zilizopatikana kwa vikwazo vya nchi yetu kufanya biashara za nchi za Ulaya kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaye mchangiaji mmoja tu Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nianze kwa kuchangia mapendekezo ya Maazimio mawili ambayo Serikali imependekeza kwamba Bunge liridhie. Moja imependekeza kwamba Bunge turidhie marekebisho haya na katika hili, naomba niungane na Kambi Rasmi ya Upinzani kusema kwamba hili Azimio kipengele hiki cha (a) iliridhie na maangalizo ama masharti. Kipengele cha (b) Serikali imependekeza kwamba Wizara ya Fedha iendelee kusimamia na kuratibu masuala yote ya kisekta. Katika hili, napenda kuungana na angalizo ambalo limetolewa na Kamati kwenye kifungu cha 2.3 kuhusiana na umuhimu wa Bunge kupata taarifa mbalimbali za majadiliano na kuhusishwa katika masuala mbalimbali na michakato inayoendelea juu ya mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, nikianza na sehemu ya kwanza ya Azimio, nimetazama kwenye mkataba tuliopewa, kifungu cha 34 na kifungu cha 36 kuna maneno yanayonifanya nihisi kwamba kuna haja ya kuridhia huu mkataba pamoja na maangalizo (*reservation).* Kwenye Ibara ya 34 ya mkataba inaonyesha kwamba matokeo ya makubaliano hayo ni pamoja na kufungua wigo wa kibiashara na kutetereka ama kumomonyoka kwa ile mifumo ya upendeleo ambayo nchi za Asia, Caribbean na Pacific ilikuwa nayo kwenye mahusiano yao ya kibiashara na *EU* na mkataba umetumia neno "*Preference Erosion".*

Mheshimiwa Spika, sasa katika mazingira kama haya na kwa kurejea maelezo ambayo Waziri ameyaeleza

Bungeni ambayo yamejikita zaidi kwenye kueleza katika kipindi cha miaka takribani 10 toka mkataba usainiwe mwaka 2000 na nchi yetu iliridhie mwaka 2001, miaka 10 imepita, mafanikio ambayo Serikali inayaeleza Bungeni ni misaada ya kifedha ambayo tumepata na sio fursa za kibiashara na kiuchumi ambazo tumepata kwenye makubaliano haya. Katika mazingira kama haya, inaonyesha miaka 10 ya Mkataba wa Cotonuo bado hatujaweza kujijenga kiuchumi kuweza kushindana na misukosuko na mikikimikiki ya uchumi wa soko wa Kimataifa na katika mazingira kama haya kufungua milango na hata kama ni katika hatua ya wao kutuongoza katika majadiliano inaweza kuathiri uhuru na hali ya wazalishaji wa nchi yetu ikiwemo wazalishaji wadogowadogo katika tasnia nzima ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye Ibara ya 63, Ibara ya 36 ya huu mkataba kuna maneno vilevile yametumika kwamba kwa kusaini haya marekebisho tutashiriki kwenye majadiliano na yametumika maneno *removing progressing barriers* yaani tutaanza vile vikwazo ambavyo sisi wengine tulikuwa tumeviweka ndani ya nchi yetu vya kiuchumi, vya kibiashara kati ya sisi na nchi za Ulaya, tutaanza kuviondoa hatua kwa hatua. Sasa napenda Serikali ituhakikishie tu kwamba pamoja na kuwepo kwa maneno haya, pamoja na kusaini makubaliano yakiwa na mwelekeo huo, bado maslahi ya kiuchumi ya nchi yatalindwa, bado hatutaingizwa kwenye Ukoloni Mamboleo na Ubeberu wa Kiuchumi kwa kutumia Mashirika makubwa ya Kimatiafa na Makampuni yao ambayo yatakuwa na athari kubwa kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kipengele (b), nakubaliana na Wizara ya Fedha kuratibu sekta nyingine. Lakini ningeshauri katika muktadha wa angalizo lililotolewa na Kamati kwenye 2.3 kuhusu Bunge kuhusishwa kwenye majadiliano na michakato mbalimbali na kwa kurejea Ibara ya pili ya Mkataba huo ambayo imekuwa bora kidogo kuliko ule mkataba wa mwanzo ambayo imeruhusu sasa kwa mara ya kwanza katika historia ya mahusiano kati ya sisi na Ulaya, Mabunge ya nchi zetu kuwa na nafasi katika ushirikiano huu, Serikali za Mitaa kuwa na nafasi kwenye ushirikiano huu, sekta binafsi na Asasi za Kiraia kuwa na nafasi kwenye ushirikiano huu.

Sasa kwa kuzingatia matakwa ya hii Ibara ya pili ya huu Mkataba ambayo leo imeletwa hapa kwa ajili ya kuridhiwa, ni vizuri kwenye Azimio hili kukawa na Sehemu C, na kutokana na ufinyu wa muda, sitaweza kuwasilisha jedwali la marekebisho; lakini Serikali ikubali kwamba iweke utaratibu wa kuwezesha Bunge, Serikali za Mitaa na Taasisi mbalimbali kushiriki katika michakato ya ushirikiano chini ya Mkataba huu, kwa kuwa hii ndiyo changamoto kubwa iliyokuwepo kwenye kipindi kilichopita cha miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulikuwa unaonekana kama ni Mkataba Kati ya Serikali na Serikali, na matokeo yake Bunge ambalo ni wawakilishi wa wananchi halikuwa na nafasi ya kutosha. Serikali za Mitaa ndizo zinazoathirika, na kuna athari nyingi zinatokea kule kwao na miradi ya maendeleo inatekelezwa kwao, hazikuwa na nafasi ya kutosha kwa maana ya asasi za kiraia, sekta binafsi, walikuwa wanaona kama Mkataba huu ni wa Kiserikali. Sasa tukiacha hii Sehemu B peke yake ya Wizara ya Fedha kuratibu sekta zote bila kuwa na pendekezo lingine la C la

kutoa nafasi kwa Bunge, kwa asasi za kiraia na kwa Serikali za Mitaa, tutaendelea na utamaduni ule ule wa zamani wa majadiliano, masuala yanayohusu mikataba hii kuendelea kwenye kivuli cha kiserikali bila Bunge, Serikali za Mitaa, sekta binafsi na asasi za kiraia kuwa na nafasi yake ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, vilevile naishauri Serikali, kwa maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri, kuna mambo makubwa matatu yanayojitokeza. Kwanza, kwa kurejea ukurasa wa pili wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja na ukurasa wa tatu, inaonyesha bayana kwamba haya mafanikio tuliyoyapata kwenye *EDF* Na. 9 na *EDF* Na. 10 yanakwisha mwaka 2013.

Kwa hiyo, kama yanakwisha mwaka 2013, inabidi kama Taifa sasa tuanze kuathiri majadiliano ya *ADF* Na. 11 yatakayoanza kuanzia mwaka 2014 na kuendelea. Hili litawezekana tu kama Serikali itaji-*commit* kama ambavyo sasa tumeletewa huu mkataba. Tutaletewa taarifa ya Serikali kuhusu *negotiation* zitakazoanza juu ya maandalizi ya *ADF* 11 ili miradi ya maendeleo ipewe kipaumbele kama tunavyoona hii miradi hapa. Miradi mingine tunaweza tukauliza, huu uliamuliwaje kuwa kipaumbele? Safari hii miradi ya kipaumbele iwe kweli tuliyoiamua Wabunge kwa kutumia vilevile Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano ili baadaye tutekeleze miradi ambayo kweli italeta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa lingine ni kwamba Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ameeleza bayana kwamba Mkataba huu kila baada ya miaka mitano unafanyiwa marekebisho. Marekebisho ya sasa kimsingi

yametukurupusha. *Negotiation* zilianza mwaka 2009 zilishika kasi sana mwaka 2010 na wakati *negotiation* zinandelea, nchi yetu ilikuwa kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, hatukuwa na nafasi ya kutosha kama Taifa kwenye *negotiation* na mkataba huu umesainiwa tarehe 29 Oktoba, 2010. Kwa hiyo, nchi iko kwenye uchaguzi, watu wanakimbizana na kampeni, kila mtu anakwenda kivyake, lakini kuna wengine wanaendelea na *negotiation* na wanaendelea na kusaini mikataba.

Mheshimiwa Spika, ili hili lisijitokeze, tunapokwenda kwenye *negotiation* za Mkataba wa mwaka 2015, ni lazima kuanzia sasa tufikirie huko tunapokwenda, na ningependa kupata kauli ya Serikali kuhusu sababu zilizofanya Serikali, Mkataba huu usainiwe Oktoba, 2010, leo ni mwezi Oktoba 2012, miaka miwili toka Mkataba usainiwe ndiyo unaletwa Bungeni. Ni kwanini Serikali imechelewa kwa miaka miwili kuleta Mkataba huu Bungeni na kifungu kimojawapo cha msingi sana cha huu Mkataba ni kuanza kuingiza malengo ya maendeleo ya milenia kwenye tasnia ya mahusiano yetu na Jumuiya ya Ulaya? Malengo ya milenia yanakwenda mpaka mwaka 2015, sisi tunakuja kuridhia Mkataba mwaka 2012: Je, tutakuwa na muda wa kutosha wa kutumia fursa za Mkataba huu kwenye kufanikisha malengo ya maendeleo ya milenia?

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu pamoja na maelezo ya mafanikio ambayo Serikali imejikita zaidi katika kueleza juu ya faida za kifedha binafsi, naona kwamba hatujapata tija ya kutosha. Kwa sababu lengo la msingi ilikuwa ni kujenga uchumi endelevu ili kupunguza na hatimaye kuondoa umaskini, sasa kwa Tanzania ukiangalia takwimu za umaskini, umaskini unazidi kuongezeka. Sasa miaka kumi

ya ushirikiano na miradi yote hii, umaskini unazidi kuongezeka, pengo la mwenyenacho na asiyenacho linazidi kuongezeka na hii inanipeleka kwenye kuamini kwamba tunapata misaada sawa, lakini ukilinganisha misaada na mapato tunayopoteza kutokana na uporwaji wa raslimali zetu, ukiangalia ripoti ya karibuni ya *one billion question*, ukiangalia ripoti nyingine za kimataifa, tunaweza kusema kwamba sisi tunapewa peremende na wenzetu wanachukua vitu vya msingi zaidi kama madini, gesi na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuhakikishiwa kwamba Mkataba huu hasa katika kifungu hiki kinachohusu ushirikiano wa kisiasa; na nashukuru kwamba kifungu hiki cha ushirikiano wa kisiasa kimeingizwa. Kifungu cha 29 ambacho kina maeneo vilevile kwamba kutakuwa na ushirikiano wa kikanda katika kukabili biashara haramu, katika kukabili rushwa, na nashukuru kwamba Umoja wa Afrika umeingizwa katika huu mchakato. Sasa ningependa Serikali wakati inapohitimisha hoja, iseme, sasa *initiative* hii, uamuzi wa kuingiza ibara hii ya 29 utatusaidiaje.

Kwa mfano, kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya kuhakikisha mabilioni yaliyoko Uswisi yanarejeshwa Tanzania kwa haraka. Mkataba huu unatusaidiaje kwenye mambo kama hayo? Kuingizwa kwa Umoja wa Afrika kwenye Mkataba huu: Je, Serikali sasa iko tayari kuleta Bungeni Mkataba wa Afrika uliosainiwa wa siku nyingi sana wa *The African Charter on Election Democracy and Governance* ambao ungeweza ukasaidia nchi yetu kuweza kukabiliana na hizi changamoto? Je ni lini nao utaletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa?

Mheshimiwa Spika, kuingizwa kwa hii ibara ya 29 ya huu Mkataba, itatusaidiaje sasa kama Taifa kuongeza kasi zaidi kurekebisha mifumo yetu ya kiuchaguzi? Tunaona tumetumia Shilingi bilioni tatu kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita kutoka Jumuiya ya Ulaya. Lakini: Je, ufanisi wa uchaguzi wetu ulikuwa sawasawa na Euro zote hizo zilizotumika kwenye uchaguzi? Haya ni kati ya masuala ya msingi ambayo tunapaswa kujiuliza na kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kwa upande wa miradi hii ya kijamii, *ADF* Na. 9 ilitekeleza mradi wa barabara ya Mandela ambao uligusa vilevile Jimbo la Ubungo, lakini mkataba ulipaswa kwisha mwaka 2009. Mradi umeendelea kwa muda mrefu, hatimaye fedha zimeongezeka zaidi na tayari kuna malalamiko kuhusu ubora wa barabara ya Mandela. Ukienda Ubongo mataa sasa hivi utakuta tayari kuna maeneo ambayo barabara imeshaanza kuharibika. Sasa ni lazima tunapofanya marekebisho ya Mkataba tuweze kuwa na mfumo endelevu zaidi. Miradi inayofuata iweze kutekelezwa kwa ufanisi ili kuweze kuwa na thamani zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwenye ukurasa wa nne, kipengele cha pili kwenye *ADF No. 10* kiasi cha fedha kinachotengwa safari hii kimetengwa Euro milioni 139 kwa ajili ya utekelezaji wa miundombinu ya usafirishaji kupitia kusaidia mpango wa bajeti wa kisekta kwa maana ya *Transport Sector Budget Support.* Ningependa kupata kauli ya Serikali katika muktadha wa mpango wa Taifa wa maendeleo wa miaka mitano kuhusiana na barabara za kupunguza foleni katika Jiji la Dar es Salaam.

Kwa kuwa sasa hii *package* inakwenda kwisha mwaka 2013: Je, katika hiki kiwango kilichotengwa cha Euro milioni 139, itajumuisha vilevile ile *package* ambayo kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kwenye mwaka wa fedha 2012/2013 ilipaswa kutengewa Shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga *ring roads* ama barabara za pembeni za kupunguza msongamano. Ningependa kupata kauli ya Serikali iwapo kwa ujumla wake Serikali itaweza ku-*team up* na wadau wengine katika kufanikisha huo mpango kupitia mpango huu.

Mheshimiwa Spika, nimeona nichangie hayo, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Umeunga mkono hoja. Haya umejaza kweli kweli! Kila kitu kimesemwa hapa! Basi Mheshimiwa Waziri atajiandaa, lakini sasa nimepata mchangiaji mwingine Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami mchana huu wa leo niweze kuchangia machache katika Azimio hili la Kuridhia Marekebisho katika Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, yangu yatakuwa ni machache hasa katika sehemu nzima ya angalizo. Ni kweli kwamba inapokuja *amendment* kama hii, lengo kubwa na maudhui makubwa ni kuboresha masuala mazima ya mahusiano na suala zima la uchumi katika nchi zetu. Lakini angalizo ambalo napenda kulitoa ni katika suala zima la mambo ya kiuchumi, lakini katika suala zima la kisera.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia katika nchi yetu ya Tanzania, hivi sasa tumepata bahati ya upatikanaji wa gesi asilia katika Bahari yetu ya Hindi. Jambo hili kama Watanzania inabidi tujitathmini vizuri. Tumepata bahati hii, lakini mpaka hivi sasa hatuna sera ya gesi na hivi sasa hatuna Sheria ya Gesi. Nini maana yake? Maana yake ni kwamba, kama Watanzania tunatakiwa tuwe mahali pazuri, tuangalie ni jinsi gani tutafanya kuweza kusimamia uchumi wetu sisi wenyewe?

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu nilionao, isije ikawa katika kuridhia kwa mkataba huu, Tanzania ikaja kushindwa kutekeleza mikakati yake ya kiuchumi, ikajikuta inapangiwa mambo, kama gesi yenu mtumie vipi. Huu utakuwa msiba mkubwa sana kwa Watanzania.

Kwa hiyo, kama Mbunge, Mtanzania, napenda kuishauri Serikali kwamba katika kuridhia hili, tuangalie jinsi gani tumejipanga kuhakikisha kwamba uchumi unaohusu Watanzania, unabaki kwa Watanzania. Maana tutakuja kuwa na kilio kikubwa sana. Leo hii tunasema rasilimali tumeigundua hapa Tanzania, isije kuwa sisi Watanzania ni watazamaji, na kwa vile tumeridhia mikataba mingine ambayo kwa lengo lake kwa makusudio ya ndani inawezekana kuna ajenda nyingine ya siri, tukajikuta tunaingia katika kitanzi kibaya sana ambapo tutaendelea kuwa maskini, omba omba na kuwaomba wenzetu wa bara la Ulaya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba kama Serikali yetu na kama Watanzania, tuweze kujitathimini katika suala zima la mahusiano ya mikataba yetu. Juzi juzi

tulikuwa tuki-*shout* sana hapa Tanzania kwamba wenzetu Jumuiya ya Ulaya baadhi ya viongozi walisema wazi kwamba hatutatoa misaada yoyote ya kifedha katika nchi zinazoendelea mpaka wakubaliane na sharti kadhaa na sharti lile lilikuwa ni kwamba, watu wa jinsia moja waweze kuoana.

Hili jambo lilikuwa ni tishio sana kwetu, na nashukuru Serikali yetu ilitamka dhahiri hadharani kwa kupinga jambo hili kwamba siyo sawasawa kwa nchi yetu. Sasa angalizo langu ni kwamba, isije ikawa katika hizi *amendment* zinazokuja, inawezekana kuna *clause* nyingine za siri tukajikuta tumeridhia jambo kesho na kesho kutwa unakataa, unaambiwa bwana, mbona mkataba wako uliridhia na hili?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema ni jambo ambalo tunatakiwa kuliangalia kwa umakini wa hali ya juu kweli kweli! Leo hii tunajikuta tumeridhia wenzetu, kumbe na haya tunaona kwenye vikao vyao walisema wazi hadharani na hata jirani zetu wa Malawi wenyewe waliridhia katika baadhi ya mambo, sisi tulikataa. Sasa kukataa kwetu, leo tunaweka *signature* tunasema tumeridhia kesho na kesho kutwa tunajikuta tumekuwa katika mazingira magumu kweli kweli katika suala zima la kuridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tunashuhudia katika kuridhia mikataba hii, tuangalie jinsi gani tunakubaliana na wenzetu kwa usawa. Tukikumbuka kabisa kudondoka kwa utawala wa Gaddafi, sisi Watanzania na Umoja wa Afrika wote, ukiangalia kwa asilimia kubwa tulikuwa na maazimio yetu kwamba ni jinsi gani tutafanya kama waafrika. Tumekubaliana kwamba tulikuwa hatujaridhia kwamba utaratibu siyo ule wa kumwondoa Gaddafi, lakini wenzetu

walikuja na maazimio yao na wala sisi Waafrika hatukuwa na uwezo wowote wa kuzuia lolote lililotokea katika nchi ya Libya. Japokuwa tunasema wamoja, lakini wenzetu wanapoamua kutekeleza ya kwao, wanatekeleza kwa uwanja mpana kabisa bila shida ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ndiyo maana nasema, katika kuridhia mkataba huu, suala kubwa ni angalizo. Jinsi gani tumejiweka? Mimi siamini kama kweli tutakuwa na ubavu mmoja tunaopimana katika mizani inayofanana. Mimi siamini hivyo kabisa! Hili maana yake litakuja kuwa kilio kwetu. Ni lazima kama Serikali ituelekeze vizuri na itueleze hapa kwamba jinsi gani katika mambo haya ya maangalizo kwa ajili ya kulinda haki ya Mtanzania na haki ya sisi tuliopo Bungeni mwisho wa siku licha ya kuridhia, lakini tutasimama katika maeneo yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, atuweke sawa ni kwa jinsi gani hii rasilimali ya gesi, suala zima la masharti ya kifedha katika bajeti zetu, la kwamba watu wa jinsia moja kuoana kama halitaweza kuguswa katika Mkataba huu na suala zima la maamuzi katika Serikali zetu tunazozifanya hasa kulinda stahili na haki zetu kama Watanzania?

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata ufafanuzi huo kwa kina, basi mimi niko radhi kuunga mkono Azimio hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Huyo alikuwa msemaji wetu wa mwisho. Nataka kuwahakikishieni kwamba Bunge linashiriki katika mikutano ya *ACP-EU* na mwakilishi wetu sasa hivi ni

Naibu Spika na kwa miaka yote tunashiriki. Kwa hiyo, kama Bunge tunashiriki. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Wabunge wote ambao wametoa maoni yao kuhusiana na kuridhia Mkataba huu wa *ACP*. Muda umeni-*empty* kwa sababu nilikuwa nataka kuchangia kuhusiana na maeneo mawili matatu. Kwanza, ushiriki wa Bunge katika hii *ACP* kama ulivyosema kwamba Bunge linashiriki kikamilifu katika majadiliano hayo kwa kutumia mwakilishi wetu Naibu Spika.

Aidha, kulikuwa na maeneo machache hususan kutoka kwa Mheshimiwa Mnyika kwamba maelezo ama manufaa ambayo yametolewa yanahusiana sana na faida za kifedha ambazo zimeonyesha wazi. Lakini tunapenda kumwakikishia kwamba hayo maeneo ambayo yameonyeshwa katika Mkataba huu ni maeneo mengi sana na tumefaidika sana. Kweli eneo moja ambalo mimi mwenyewe nilishiriki binafsi, hususan ujenzi wa Bandari ya Zanzibar, tulipata karibu Euro milioni 42 kwa ajili ya ujenzi huo.

Kwa hiyo, tumesaidiwa *infrastructure* lakini utekelezaji na ukamilishwaji wa ile bandari umesaidia uchumi wa Afrika Mashariki kwa ujumla, sio Zanzibar tu. Kwa hiyo, utaona kwamba hata ile *infrastructure* ambayo tumesaidiwa *through financing* ya *42 million* imefaidisha uchumi wa Tanzania na uchumi wa Afrika Mashariki.

Vilevile kumetolewa faida nyingine ambayo imepatikana ya kifedha *three million Euro* kwa upande wa Zanzibar, lakini wenyewe una *strengthen capacity* ya *non*

*state actors* kushiriki katika *policy dialogue.* Kwa hiyo, yenyewe inawezesha *non state actors* kushiriki katika *policy dialogue* za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo *direct financing* lakini vilevile *outcome* yake itasaidia ushiriki wa *non state actors* katika ku-*sharpen* sera za nchi hii ziwe za kiuchumi, kisiasa, na maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, hilo pia ni eneo lingine ambalo tumefaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu majadiliano katika *ADF 11* inayokuja, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wabunge walishiriki katika majadiliano hayo ya mwanzo ambayo yalifanyika mwezi Mei mwaka huu 2012 na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla siku hiyo ya majadiliano ndiyo siku ambayo kulifanyika marekebisho ya Baraza la Mawaziri. Mimi ni mmojawapo kwa upande huu nilikuwa natoka Zanzibar kama mwakilishi wa Wizara ya Fedha, lakini ndiyo siku ambayo niliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Fedha.

Kwa hiyo, nina *evidence,* hata Mheshimiwa Waziri naye alishiriki katika majadiliano hayo ya *ADF 11* na tume-*discuss* sana na bado majadiliano yatakuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, mimi yangu ni hayo machache naomba Mheshimiwa Waziri aendelee. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja, Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru mzungumzaji kwa niaba ya

Kamati ya Fedha na Uchumi kwa ushauri wao mzuri waliotushauri katika hitimisho lao. Nilishatoa shukrani, lakini wameongezea katika hii taarifa yao. Wamezungumza umuhimu wa Wizara ya Fedha kuwa macho katika kusimamia na vilevile kufanya tathmini. Tunakubaliana na ushauri huo wote.

Pili, nachukua nafasi hii kushukuru vilevile mawazo ya Kambi ya Upinzani, wamekuja na mawazo mazuri, lakini tunahitaji kusaidia kutoa ufafanuzi pale ambapo tunafikiri panahitaji kuboresha mawazo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwamba hakuna ushahidi kwamba nchi za Afrika zinanufaika isipokuwa pengine nchi za Ulaya ndiyo zinanufaika, hoja hii inaweza isiwe na ukweli, kwasababu nilipokuwa ninawasilisha hapa, kwanza nimeeleza maeneo na madhumuni ya Mkataba na namna Mkataba ule ulivyotusaidia mpaka dakika hii kama wanachama wa nchi husika.

Nimesema madhumuni ya kwanza ya Mkataba ule ni kujenga uchumi endelevu; pili, kuimarisha miundombinu yetu ya kimaendeleo ya kifedha; na tatu, biashara na vitega uchumi pamoja na kuimarisha *political dialogue,* yaani majadiliano ya kisiasa katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, inawezekana katika *partinership* ya namna hii hata Ulaya wananufaika kwa namna moja au nyingine, lakini kwa takwimu tulizonazo sisi kama Serikali, nchi zetu hasa Tanzania tumenufaika kwa sehemu kubwa kama nilivyowasomea yale niliyowasilisha, na nilifanya makusudi ili Waheshimiwa Wabunge wapate picha kwa miaka hii ni maeneo gani nchi yetu imenufaika kupitia mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna ushahidi wa kutosha kabisa kuwa nchi yetu imenufaika. Kwa hilo halina shaka. La pili, limetoka kwenye hoja ya Mheshimiwa Mnyika, amezungumza mambo mengi mazuri ya kiushauri ambayo Serikali tunachukua ushauri wake mzuri.

Kuna mambo fulani ambayo ni lazima nifanye maelezo ya ziada. Kwa mfano, hili la kwamba tulichelewa kuleta Bungeni, ni sahihi. Kama Serikali ili-*sign* mwaka 2010 na tunaleta leo mwaka 2012, ni kweli kuwa muda umepita. Lakini Waheshimiwa Wabunge kuna hatua kadhaa ambazo ni lazima zifuatwe kabla ya kuridhia Azimio lolote lile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa muda ule wa kutathimini na kuona kama Azimio lina-*side effects,* ndiyo huwa tunachukua na kuangalia na tunapojiridhisha kuwa hakuna *side effects* ambazo zinaweza kuleta athari kwa nchi yetu, ndipo tunaleta Bungeni kwa maridhio, na hiyo imekuwa baada ya hatua za uchunguzi.

La pili, Mheshimiwa Mnyika amezungumza kwamba manufaa tunayosema Mkataba huu unaweza ukawa unajenga uchumi endelevu na kuelekea kupunguza umasikini, kwa takwimu zake au kwa upande wake anaona umasikini unaongezeka kuliko unavyopungua. Kwa taarifa, katika kipindi cha mwaka 2001- 2010, ni kweli uchumi ume-*grow* kwa wastani wa 7% yaani *GDP gross rate* imekua kwa wastani huo wakati ukitazama takwimu za umasikini kutoka mwaka 2000 – 2011. Mwaka 2011 ilikuwa 35.6% wakati mwaka 2012 imekuwa 33.4%. Kwa hiyo, umasikini ukapungua kwa 2.1%.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa uchumi umeongezeka katika hiyo *rate* kubwa, lakini ni kweli vile vile kuwa umasikini umepungua, lakini siyo katika *rate* ya namna uchumi ulivyokuwa una-*grow.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sahihisho ni kwamba, umasikini umepungua katika *speed* ndogo ukilinganisha na ukuaji wa uchumi. Lakini siyo kweli kuwa umasikini badala yake umekuwa ukiongezeka, kwa hiyo, hii nimeona niiweke vizuri kwasababu ni takwimu halisi tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba Wizara ya Fedha imechukua jukumu la kuratibu utekelezaji; kwa nini isiachie na ngazi nyingine zikafanya kazi hii? Tunachozungumza sisi ni ngazi ya uwajibikaji katika ngazi kuu ya Serikali, Wizara ya Fedha iratibu, lakini ushirikishwaji kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mnyika ni sahihi, ushirikishwaji katika *Local Goverment Authiority* pamoja na sekta na sekta nyingine ni lazima zishiriki ili mchakato uweze kuwa *inclusive.* Hili ni pendekezo zuri, lakini uwajibikaji wa kuratibu utabakia ngazi ya Wizara ya Fedha kwasababu ni lazima tuwe na *champion.*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyika amezungumza vile vile kwamba ibara ya 63 inayozungumza *removing progressively barriers,* haina maana ya kwamba sasa tunarudi kwenye ukoloni wa kisasa. Tunazungumzia namna gani tutapunguza mazingira ambayo pengine kwa kuwepo kwake yanatufanya tusiwe na biashara endelevu ya kushirikiana na nchi ndani ya wanachama, lakini tunakuwa

waangalifu kila hatua tunapofungua *barriers* bila kuathiri haki na usalama wa nchi zetu.

Lingine Mheshimiwa Mnyika amezungumzia kuwa pengine misaada tunayoizungumza imekuwa ni misaada ya michango, lakini siyo fursa za kiuchumi. Unapopata misaada katika *GBS* yaani *General Budget Support,* ukaelekeza pesa zile katika miradi halisi ambayo ina *impact* halisi kwa wananchi, basi siyo kwamba umepata misaada peke yake, lakini pia umepata msaada wa kutatua tatizo na ndicho hicho ambacho sisi tumepata.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwamba ni namna gani misaada ile tuliyopata ilivyoleta manufaa. Misaada ile imetusaidia katika *General Budget Support,* imetusaidia kwenye *STAPETS,* nimeeleza kwa kirefu, imetusaidia katika elimu, imetusaidia katika kuboresha bandari hata pale Zanzibar, imetusaidia vile vile katika Utawala Bora. Hayo yote siyo neno, misaada peke yake lakini ni misaada iliyofika mahali ambapo pameleta *impact* kwa wananchi katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nichukue nafasi hii vilevile kumshukuru Mheshimiwa Said Jafo kwa mchango yake na ushauri ambao ametupa.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wa kuzungumza walikuwa wawili, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Said Jafo ukiacha Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani. Wote kwa pamoja ninawashukuru sana kwa mawazo yao na ushauri wao mzuri na Serikali imechukua. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mwongozo!

**SPIKA:** Mwongozo, kaa kwanza, hoja hii imeungwa mkono Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kusimama hapa kwa Kanuni ya 68(7) kuhusu mwongozo wako, lakini ninataka kusimamia Kanuni ya 77 kwamba kabla hujalihoji Bunge hili kuhusu kupitisha Azimio hili naomba uangalie akidi ya hili Bunge.

**SPIKA:** Niangalie nini?

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nusu ya Wabunge haijatimia. Idadi ya Wabunge, yaani akidi ya kupitisha Azimio haijatimia. Hilo la kwanza.

La pili, taarifa ya Kamati hii ambayo imesomwa kuhusu Azimio hili, ni ndogo mno na kuna taarifa kwamba ni watu wanne tu waliohudhuria katika Kamati kupitisha hili.

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu, Azimio hili ni nyeti, linalohusiana na Uchumi na Ushirikiano wa Kikanda ambapo kwa kuwa taarifa ya Kamati ndiyo hivyo fupi na haijapewa ufafanuzi mzuri na tumepewa kabrasha hili sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu zote tatu hizo, naomba utumie mwongozo wako na busara yako ili Azimo hili lisipitishwe leo, itafutwe siku nyingine Waheshimiwa Wabunge watakuwa wameshapitia vya kutosha. Naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mwongozo wangu ni kwamba hili Azimio tutapitisha kesho asubuhi, lakini hatujadili kwa sababu moja tu kuwa akidi kweli haitoshi. Maelezo mengine hayana msingi kwa sababu Kamati inayohusika ndiyo yenye mamlaka ya kumwandikia Spika kuwa tumepitia taarifa yetu hii na tumekubali kuwa tumeipitisha na kuwa iingie katika Bunge. Kamati ya Uongozi jana imefanyia kazi masuala yote haya katika hoja ambayo ilikuwa iko tayari siku nyingi. Kama wewe hukusoma, hilo ni tatizo lingine. Nakubaliana na wewe tu kuwa ukumbi huu hautoshi kupitisha hoja hii sasa. Kwa hiyo, tutakapokutana hapa tutawahoji wanaoafiki, basi. Lakini siyo hayo mengine unayoyaeleza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hivi naomba tukutane kwenye Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya *briefing* ambayo ni ya kawaida. Tulishindwa kufanya jana kwa sababu Kamati ya Uongozi ilikuwa haijapitia kazi yake. Kwa hiyo, ninaahirisha Kikao cha Bunge mpaka hapo kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.10 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 31 Saa Tatu Asubuhi)*